**Ajali** zilivyoua watu wanane wakiwamo wanafunzi
UKURASA 2

**Othman:** Mabadiliko demokrasia, uchumi haki ya wananchi
UKURASA 5

**MAISHA:** Unayomtendea mwenzako nawe utatendewa
UKURASA 11


# Nipashe JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0581786
Jumapili Septemba 1, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




**SANCHO ATUA CHELSEA**
UKURASA 22

RIPOTI MAALUM

# Sheria, pombe lugha gongana



**WATOTO** rukhsa kunywa miaka 15, vileo vyauzwa kila kona; shisha, sigara usipime ...
*Endelea ukurasa. 4*




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akikabidhi zawadi kwa mmoja wa washindi wa mashindano ya Dunia ya Qur'an Tukufu kwa Wanawake (katikati), yaliyofanyika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Wazee wa mila, waganga wa jadi wacharuka utekaji, watu kupotea
UKURASA 3

## Wapinga kifungu sheria rushwa ngono
UKURASA 2

**MICHEZO** MAXI AFURAHIA REKODI YA MAYELE UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Hemed ataja vikwazo maendeleo Zanzibar

**Na Maulid Mmbaga**

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema changamoto kubwa zinazoisumbua Zanzibar ni kiwango kikubwa cha umaskini wa mahitaji muhimu pamoja na ukosefu wa ajira kwa vijana.

Hemed aliyasema hayo jana visiwani Zanzibar, wakati akifungua kongamano la kukusanya maoni ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

Kutokana na changamoto hizo, Abdulla aliwataka wananchi kufikiri kwa kina namna ya kutatua changamoto mbalimbali za kijamii, pamoja na kutoa maoni yao kuhusu namna bora ya kuimarisha ustawi wa taifa.

"Tunapaswa kupanga na kuweka mikakati imara ya kuendelea katika matazamio ya muda mrefu kwa faida ya kizazi kijacho. Dira ya Maendeleo ya Taifa inayoandaliwa ni ya watanzania wote na si ya serikali ama ya chama fulani," alisema Abdulla.

Alisema athari za mabadiliko ya tabia nchi, udumavu wa watoto kwa zaidi ya asilimia 30 na ukuaji mdogo wa matumizi ya teknolojia ni mojawapo ya masuala ambayo yamekuwa yakitatiza kasi ya maendeleo visiwani humo.

Abdulla aliomba wadau wa maendeleo, taasisi za umma na sekretarieti za mikoa, kuendelea kutoa maoni yao katika mchakato wa uandishi wa Dira Mpya, ili kuhakikisha inaakisi maoni ya wananchi.

Kwa upande wa timu ya kitaalam ya kukusanya maoni ya Dira Mpya, ilisema watanzania wengi wanataka serikali kujenga uchumi madhubuti, jumuishi, endelevu, shindani na stahimilivu katika jitihada za kupambana na umaskini.

Mhadhiri wa chuo kikuu Zanzibar na Mjumbe wa timu hiyo, Dk. Yahya Hamad Sheikh, alitaja maeneo mengine yaliyotajwa zaidi na wananchi, kuwa ni pamoja na maboresho katika huduma za kijamii, ikiwamo katika sekta ya afya, lishe, elimu, makazi bora na upatikanaji wa majisafi na salama.

Hamis Mnubi, mkazi wa Zanzibar, alishauri kuwa miaka 25 ijayo, kunatakiwa kuwa na uimara utawala bora, upatikanaji wa haki, ulinzi na usalama wa taifa pamoja na maendeleo ya sayansi, teknolojia na uvumbuzi kama sehemu ya kuharakisha maendeleo.

"Tunataka kuanzia sasa mpaka 2050, umeme usizimike tena Tanzania, kwa kuwa tumealika wawekezaji, tunajenga maghorofa yenye teknolojia ya umeme.

"Tuna treni ya kisasa SGR, hatutaki kusikia tena imekwama kwa sababu ya umeme," alisema.



Ofisa Usafi na Mazingira wa Manispaa ya Kinondoni, Alban Mugyabuso (wa pili kushoto), akishirikiana na makundi mbalimbali, kufanya usafi wa mazingira katika Zahanati ya Kijitonyama, Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Wapinga kifungu sheria rushwa ya ngono

**Na Mary Geofrey**

WANAMTANDAO wa Kupinga Rushwa ya Ngono Tanzania, wamepinga muswada wa mabadiliko ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Ngono, Kifungu cha 10(b), unaotarajiwa kusomwa bungeni Jumatatu (kesho), kwa madai kinahalalisha rushwa ya ngono kwa vijana na wasichana.

Aidha, mtandao huo unasisitiza kifungu cha 25 katika sheria hiyo inajitosheleza na hakihitaji marekebisho yoyote na kiendelee kutumika, hivyo kifungu 10 (b) kiondolewe.

Mmoja wa wanamtandao hao, Rebeca Gyumi, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu muswada huo wa sheria.

"Hoja ya msingi wa kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kinaeleza kuwa ili kuwe na rushwa, lazima kuwe na mtoaji na mpokeaji. Kwa nini rushwa ya ngono inamwangalia mpokeaji tu?" alihoji.

Gyumi aliwaomba wabunge kutopitisha muswada huo, kwa ajili ya maslahi mapana ya waathirika wa rushwa wa ngono nchini. "Sisi wanamtandao tunataka wanaoendelea kupigia debe mabadiliko haya, wasipotoshe umma kwa kuchanganya dhana ya rushwa, mshawishi, anayeshawishi na anayeshawishika," alisema Gyumi.

Mwanamtandao na Mwanaharakati, Dk. Ananelia Nkya, alisema, "Wabunge wakipitisha kifungu hicho, wataliangamiza taifa kwa kuhalalisha matukio ya rushwa ya ngono."

Alisema muswada huo pia ukipita si tu utadhalilisha utu wa wanaofanyiwa ukatili wa rushwa ya ngono, bali pia unamdhalilisha Rais Samia Suluhu Hassan.

Wanamtandao hao na washiriki wote wanaopigania haki za binadamu na makundi ya pembezoni, kutoka takribani asasi 200 kuanzia ngazi ya jamii hadi taifa.

Mtandao huo pia, ulihusika na uchambuzi yakinifu wa mapendekezo ya awali ya marekebisho ya sheria hiyo na kutoa tamko lao kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

# Ajali zilivyoua wanane wakiwamo wanafunzi

**Na Waandishi Wetu**

WATU wanane wakiwamo wanafunzi watatu wamefariki dunia katika ajali zilizotokea mikoa miwili tofauti baada ya magari waliyokuwa wakisafiria kugongana uso kwa uso na mengine.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Ahmed Makarani, alisema watu wanne wamefariki dunia jana wilayani Babati baada ya gari la mizigo aina ya Scania kuligonga basi dogo aina ya Toyota Coaster lililokuwa na wanafunzi hao.

Alisema ajali hiyo ilitokea eneo la Gajal, wilayani Babati na kwamba chanzo chake ni Scania kuligonga basi hilo dogo lililokuwa likitokea wilayani Hanang' kwenda Arusha, likiwa na wanafunzi 33.

"Dereva wa lori alikuwa mzembe kwani alishindwa kuwa makini barabarani na kuligonga basi dogo na kusababisha vifo hivyo," alisema Makarani

Alisema wanafunzi watatu waliokuwa kwenye basi hilo dogo walifariki dunia pamoja na dereva.

"Wanafunzi hao waliokuwa katika basi dogo walikuwa wanatoka Shule ya Sekondari Endasak wakienda likizo Arusha, baada ya shule zao kufungwa,"alisema.

Mkuu wa Mkoa huo, Queen Sendiga, alitoa pole kwa wanafunzi, walimu, wazazi, walezi na wananchi kwa ujumla kutokana na ajali hiyo.

"Tunamuomba Mwenyezi Mungu, awape nafuu na uponyaji wa haraka majeruhi wote wa ajali hiyo ambayo imesababisha vifo vya watu wanne," alisema Sendiga.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, alisema watu wanne akiwamo dereva wa gari, wamefariki dunia katika ajali iliyotokea Kijiji cha Manchali baada ya gari hilo kugongana uso kwa uso na lori.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva kutaka kulipita gari walilokuwa wakiongozana nalo na kukutana uso kwa uso na lori.

"Watu hao walikuwa wakirejea nyumbani wakitokea katika sherehe, dereva wa gari hilo, Emmanuel Kazimoto (38) pamoja na abiria wengine wawili wamekufa papo hapo, huku abiria mwingine amefariki dunia akipatiwa matibabu. Miili yao imehifadhiwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma," alisema.

Kamanda Katabazi alisema Jeshi la Polisi linaendelea kufuatilia madereva wazembe ambao husababisha ajali kwa kuendesha mwendokasi bila kufuata sheria za barabarani.

**- Imeandikwa na Jaliwason Jasson (BABATI) na Renatha Msungu (DODOMA)**

# Wazee wa mila, waganga wa jadi wacharuka utekaji, watu kupotea

**Na Waandishi Wetu**

MATUKIO ya kupotea na utekaji wa watu maeneo mbalimbali nchini, yamewaibua wazee wa mila, machifu na waganga wa jadi na kueleza kuwa kinachofanyika ni udhalilishaji wa utu na kuliletea taifa sifa mbaya.

Makundi hayo ya watu yameibuka baada ya mapema wiki hii, Jeshi la Polisi kutangaza kuwashikilia watu kadhaa, akiwamo mganga wa kienyeji, huku miili ya watu 10 ikifukuliwa mikoa tofauti nchini baada ya kudaiwa kuuawa na watuhumiwa hao.

Baadhi ya miili hiyo ilikutwa imezikwa kwa mfumo wa kukaa na wapo watoto wa watuhumiwa akiwamo mtoto wa mganga huyo wa kienyeji ambao walizikwa hai katika zizi

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti katika maeneo mbalimbali, baadhi ya wazee wa kimila na waganga wa jadi, wameomba serikali kufanya ufuatiliaji wa kina dhidi ya waganga wanaofanya ramli chonganishi na kuwachukulia hatua za kisheria.

Mkoani Shinyanga, Salumu Zarua alisema: ""Kupotea kwa watoto na utekwaji wa watu ni kulidhalilisha taifa kwamba hakuna amani tena na vyombo vya ulinzi na usalama havipo. Sisi wazee tunaomba serikali iamke kudhibiti vitendo hivi."

Mganga wa jadi, Elias Tungu, alisema matukio mengine ya kupotea kwa watoto yanahusiana na imani za kishirikina ambayo husababishwa na waganga wa kienyeji. Aliiomba serikali ifanye msako wa kuwabaini waganga ambao wanapiga ramli chonganishi na wale wasio la leseni.

Kutokana na kuwapo kwa matukio hayo, alitoa wito kwa wazazi kuwa makini na watoto wao kwa kufuatilia mienendo yao hasa wanakocheza na kuacha kuwatuma dukani nyakati za usiku.

"Katika mkoa wa Shinyanga kwa mwaka huu, tayari kuna matukio manne ambayo yamehusika watoto kupotea, huku mmoja akipatikana akiwa ameuawa kwa kukatwa viungo vyake," alisema.

**UCHAGUZI SABABU?**

Mkoani Mwanza wazee wa kimila walisema vitendo hivyo, vinatokana na watu wanaotumia kivuli cha kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.



Chifu wa ukoo wa Wahejiu wa kabila la Warimi, wilayani Ikungi, mkoani Singida, Thomas Mgonto (katikati), akionesha mkuki na ngao wakati wa maadhimisho ya sikukuu ya kichifu, katika Kata ya Siuyu, hivi karibuni. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

Walisema vitendo hivyo vinatakiwa kukomeshwa haraka iwezekanavyo kwa kuwa kuendelea kwa matukio hayo ni ukiukwaji wa haki za binadamu.

Katibu wa Machifu Tanzania, Aron Mikomangwa, alisema uchaguzi wa serikali za mitaa hauwezi kusababisha ukatili huo, bali kuna watu wanatumia mwamvuli huo kuteka watoto.

"Mwenyekiti wa mtaa yeye anajitolea hana chochote cha kupata hadi akafanye utekaji wa watoto? Wako wanaofanya unyama huo, hususani wanasiasa wa uchaguzi mkuu, wafanyabiashara wa madini. Watu wanaotafuta utajiri na wanaouza viungo vya binadamu. Hao ndio wanaoshirikiana na waganga waovu kuchafua amani," alisema.

Alisisitiza kuwa hakuna uganga unaoelekeza kuteka watoto au vitendo vya kihalifu, bali kuna waganga wasiyofuata maadili na wananchi wenye uchu wa utajiri na madaraka, wanafanya mambo hayo kwa matakwa yao kwa kukosa utu na hofu ya Mungu.

"Sisi machifu ndio walezi wa waganga. Tunatamka hatuungani na mganga yoyote anayetoa maelekezo ya wateja wao kufanya ukatili wowote, hivyo tunaiunga mkono serikali iwakamate na itoe adhabu kali kwa yeyote atakayeonekana amekwenda kinyume cha maadili," alisema.

**WAKAMATWE**

Chifu wa Mkoa wa Dodoma, Mazengo wa Pili, aliitaka serikali kuendesha operesheni maalum ya kusaka waganga wasio na leseni na kuwachukulia hatua za kisheria.

Mazengo alisema wakiwa viongozi wa kimila, wanalaani mauaji na utekaji wa watu, vitendo ambavyo vinaendelea kujenga hofu miongoni mwa watanzania.

"Sisi umoja wa machifu Mkoa wa Dodoma, tunalaani vitendo hivi na tunaiomba serikali kuchua hatua kwa waganga wa kienyeji ambao watabainika kuhusika katika matukio haya ya mauaji na utekaji," alisema.

Alisema kutokana na vitendo hivyo, wamechukua hatua za kukabiliana navyo kwa kuunda vikosi vya sungusungu ambapo kila baada ya nyumba kumi atakuwapo kiongozi.

"Hii itasaidia kila mgeni anayeingia katika maeneo yetu anajulikana anatoka wapi, kazi yake ni ipi, ili kukabiliana na vitendo vya utekaji na mauaji," alisema.

Naye Katibu wa Umoja wa Machifu Dodoma, Ndahani Chinang'anang'a, alisema wanalaani vitendo hivyo kwa sababu hivi sasa jamii inaishi kwa hofu kubwa kutokana na matukio hayo.

Chinang'anang'a alisisitiza haja ya serikali kupitia vyombo vya ulinzi na usalama kuchukua hatua stahiki ili kukomesha hali hiyo.

Chifu wa Ukoo wa Wahejiu wanaotokana na kabila la Warimi, Ikungi mkoani Singida, Thomas Mgonto (pichani), alisema matukio ya mauaji kutokana na imani za kishirikina hayakubaliki katika jamii yeyote ile.

"Sisi kama machifu hatukubaliani na matukio haya, tunapinga na tunalaani vitendo, hivyo kwani jamii yeyote ile hata kama haijastaarabika, hata kama haina elimu, hata kama haifahamu lolote utu wa mtu, uhai wa mtu ni jambo la muhimu sana katika ustawi wa himaya yeyote," alisema.

Chifu Mgonto alisema wao kama viongozi wa kimila ifahamike kuwa hakuna mila yeyote katika jamii iwe ya Wanyaturu ambayo inaweza kukubaliana na vitendo vya mauaji ya watu, kwani mila zao zimenyooka.

Alisema ili kukomesha vitendo hivyo, serikaii na taasisi zote zisizo za kiserikali waendelee kukemea vitendo hivyo na wananchi wawe wanatoa ushirikiano kwa vyombo vya ulinzi na usalama, kwa kutoa taarifa za watu wanaowahisi.

Pia alisema serikali na taasisi zisizokuwa za kiserikali, zisaidie kutoa elimu kwa wananchi, kuachana na imani potofu kwamba, kuua mtu na kuchukua viungo vya binadamu watapata utajiri.

"Watu wanaweza kusema haya yanayotokea ni mambo ya kimila hapana. Ni mambo ya watu binafsi ambao wanaingia katika mgongo wa kimila. Tunataka jamii yetu ielimishwe, ifahamu hasara ya kufanya vitendo hivyo ambavyo kimsingi, vinaharibu mila na desturi za kitanzania," alisema.

Chifu wa Unyahati, Adamu Gwau, alisema kutokana na matukio hayo,machifu wa Mkoa wa Singida wamepanga kukutana kujadiliana na kuweka mikakati itakayosaidia kukomesha vitendo hivyo.

"Matukio haya yamedhihirisha ni jamii yetu ndio inahusika, hivyo sisi kama machifu tuwe wakali kukemea mambo haya," alisema.

Mzee wa Mila Wilayani Mbarali, mkoani Mbeya, Keya Kashu, alisema pamoja na kuwapo kwa matukio hayo kuna tetesi kwamba wanaohusika na kuwatoa watu viungo ni shinikizo la watu wanaonunua figo kutoka nje ya nchi.

Kashu alisema pamoja na kwamba, waganga wa kienyeji wanachangia kutokana na masharti kwa baadhi ya wagonjwa, lakini kipindi cha nyuma walikuwa wanahitaji zaidi viungo vya albino, lakini serikali imepigana na matukio hayo kupungua.

"Ni jambo linalopaswa kukemewa na ni uonevu, ukatili na unyama mkubwa unaotia hofu. Sisi wazee wa mila tunatetea kwa nafasi yetu, lakini serikali inapaswa ifike hadi ngazi za chini katika jamii kuongea na mwananchi mmoja mmoja ili kupata suluhu ya kudumu" alisema Kashu.

Alisema wako wananchi wanaojua wahusika wa matukio hayo katika ngazi za chini, lakini kwakuwa ushirikiano ni mdogo kutoka serikalini wanaamua kukaa chini.

Wazee wa kimila mkoani Tabora akiwamo Mohamedi Thabith (70) alisema, "Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwakani, watu wameanza kujipanga kutafuta nafasi za uongozi na kuna watu nao wanatumia mwanya huo kujifanya ni waganga, ili wapate fedha wakati sio wataalamu. Ndiyo hawa wanatuleta mabalaa haya kwa kuwatuma watu wawaletee watoto ana viungo vyao."

**- IMEANDALIWA na Paul Mabeja (Dodoma), Marco Maduhu (Shinyanga), Rose Jacob, (Mwanza), Thobias Mwanakatwe (Singida), Beny Kingson (Tabora) na Halfan Chusi (Dar)**

# Pombe, sheria lugha gongana

## -Rukhsa watoto kuanzia miaka 15 kunywa, vileo vyauzwa kila kona; shisha, sigara usipime




Mratibu wa Kinga ya Magonjwa Yasiyoambukiza katika Wizara ya Afya, Goodluck Tumaini akizungumza katika kongamano la elimu na uelewa kuhusu magonjwa yasiyoambukiza lililoandaliwa na Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA), jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: ROMANA MALLYA**

**Na Romana Mallya**

NI lugha gongana. Ndivyo inavyoweza kuelezwa kutokana na sheria za nchi katika suala zima la umri wa kijana kuanza kutumia kilevi kama pombe na sigara.

Sheria za Tanzania zinaruhusu mtu mwenye umri kuanzia miaka 15 kuanza matumizi ya pombe, lakini wazalishaji wa bidhaa viwandani wameweka masharti kwamba: "Hairuhusiwi kutumiwa na kijana chini ya miaka 18."

Kukiwa na rukhsa hiyo ya kisheria (Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Pombe ya Tanzania ya Mwaka 1968) kwamba bidhaa hiyo inaweza kuuzwa kwa watu wenye umri wa kuanzia rika hilo, Sheria ya Ulinzi wa Mtoto ya Mwaka 2009 inaelekeza wazazi na walezi kuwalinda watoto dhidi ya tabia hatarishi, ikiwamo na unywaji wa pombe.

Wakati sheria zikielekeza pombe iuzwe katika maeneo maalum na kuwa na umbali wa kilomita moja kutoka baa moja kwenda nyingine, pia kukiwa na maelekezo ya muda maalum kuuza kilevi hicho, kinachoshuhudiwa mtaani hivi sasa ni lugha gongana kati ya pombe na sheria.

Mratibu wa Kinga ya Magonjwa Yasiyoambukiza katika Wizara ya Afya, Goodluck Tumaini, anasema Tanzania ina sheria ya zamani ya pombe, hivyo serikali inaendelea kuifanyia utaratibu.

"Tuna Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Pombe ya Tanzania ya Mwaka 1968. Ukisoma sheria ile imeweka leseni mbalimbali. Leseni namba moja ni ya kioski, namba mbili ya maduka ya kawaida, namba tatu ni ya baa, namba nne ni ya klabu na namba tano inahusu hoteli. Sheria inasimamiwa na halmashauri," anasema.

Anasema sheria hiyo inaruhusu mtu kuanza matumizi ya pombe kuanzia umri wa miaka 15 na zaidi.

"Kwa Tanzania tuna wanywaji wachache wanaokunywa pombe lakini wanakunywa sana lita 10.4. Hiki ni kiwango kikubwa sana cha pombe lakini kuanzia umri wa miaka 15. Kwa hiyo, ukimkuta kijana wako wa miaka 15 anakunywa, usianze kupambana naye, tuna wajibu wa kutoa elimu.

"Lakini sheria inasema usiuze pombe kabla ya muda wa saa 10, lakini leo hii kuna baa zipo kama hospitali watu wanaingia shift (zamu) nne, haijawahi kufungwa kaunta," anasema.

"Hata kama sheria ni ya mwaka 1968, lakini imekataza. Sheria imekataza kuchanganya unga, sukari, juisi na pombe. Leo hii kuna vioski vya 'Kwa Mangi' watu wengi wanakaa pale.

Kadhalika, anasema sheria inamtaka anayefungua baa, asiweke muziki wa kuvutia watu na duka la pombe kati ya duka moja na lingine liwe kilometa moja.

"Leo hii kuna baadhi ya mitaa ukienda nyumba, baa, nyumba, baa, nyumba, baa. Hata kama ulikuwa huna mpango wa kunywa utakunywa tu. Sheria hiyo hiyo inakutaka nje ya wewe, usiweke mziki, lakini mtoto asipite katika eneo la pombe, leo hii ukienda katika baa unakuta watu wapo bwaaa.

"Sheria hii imeruhusu unywe pombe asubuhi kwenye leseni namba tano ya hoteli peke yake, lakini ukinywea kwenye hoteli uende ukanunue uingie chumbani ujifungie unywe pombe yako na ukimbughuzi yeyote yule umevunja sheria," anasema.

**POMBE DAWA YA KULEVYA**

Tumaini anasema upatikanaji wa pombe umekuwa rahisi ndani ya nchi na kusisitiza kuwa kuwa pombe ni dawa za kulevya kama dawa nyingine na tumbaku zote zinasababisha ugonjwa unaoitwa uraibu.

"Uraibu ni ugonjwa kama magonjwa mengine. Ugonjwa sugu wa ubongo unaojirudia rudia unaosababisha mtu kupoteza thamani yake ndani ya jamii. Akianza kuwa na uraibu, atauza vitu ili tu akanunue pombe au tumbaku au dawa za kulevya," anasema.

Hata hivyo, Tumaini anakumbusha kuwa huduma za matibabu zipo na wataalam wote wamejengewa uwezo.

Kuhusu sigara na pombe anasema zote zina madhara yake na kila moja ina sheria.

"Sigara ina Sheria Namba 121 ya Mwaka 2003 ya kudhibiti matumizi ya tumbaku na bidhaa zake na kanuni zake za mwaka 2014. Sheria hii ukisoma Kifungu cha 24 hadi 29 inazungumza masuala ya udhibiti wa matumizi ya tumbaku na bidhaa zake na kuwataka wanaouza kuweka maeneo maalum," anasema.

Tumaini anasema ni muhimu kuendelea kuhimiza anayekaa karibu yako na kuvuta tumbaku anafanya kosa la kisheria.

**SHISHA, SIGARA BALAA**

Anasema changamoto kubwa iliyoko katika bidhaa hizo, wakati ambao sasa kuna shisha na sigara za kieletroniki, imekuwa ni ngumu kwa mzazi au mlezi kugundua kama mtoto wake anavuta, kwa sababu nyingine zimetengenezwa kama kalamu.

"Changamoto nyingine ni matumizi ya shisha yaliyopitiliza, huku sheria yetu haijazungumza masuala ya shisha. Changamoto kubwa inayotokea sasa ni pamoja na kuchanganya dawa za kulevya katika shisha.

"Unaweza kukaa na anayevuta shisha, wewe unakunywa bia zako, ukifika nyumbani hata mlango wa choo hukumbuki, umevutishwa," anasema.

Tumaini anawataka waandishi wa habari wakafanye habari za uchunguzi kuhusu mambo hayo na kuelimisha umma kuhusu matumizi ya bidhaa za tumbaku zikiwamo shisha, sigara za kieletroniki na pombe kwa kuonesha hatari iliyoko mbele yao.

Mkurugenzi Msaidizi wa Magonjwa Yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya, Dk. Omari Ubuguyu, anasema matumizi ya tumbaku yamepungua kwa sasa kulinganisha na huko nyuma.

"Matumizi ya sigara yamekwenda chini katika watu wenye umri mdogo. Lakini katika kundi la vijana umri wa miaka 18 kuendelea wanatumia katika mtindo wa shisha na bahati mbaya wanatumia sigara nyingi zaidi kwa kutumia shisha ambazo zimewekewa ladha tofauti," alisema.

"Matumizi ya pombe yamevuka kiwango Tanzania. Takwimu za dunia kiwango cha utumiaji wa pombe Tanzania kinazidi kiwango cha utumiaji wa pombe Urusi.

"Takwimu za sasa zinaonesha matumizi ya kiwango cha pombe kinachotumika Tanzania kinazidi cha Russia. Kama utachukua pombe yote inayotumika na kugawanya kwa raia wote watu wa miaka 15 na zaidi. Watu wenye umri mkubwa zaidi Urusi (Russia) ni wengi zaidi kuliko huku kwetu. Sisi watu wenye umri mdogo miaka sifuri hadi 14 wanakaribia asilimia 40 ya watu wote.

"Kwa hiyo wenye umri mdogo ni wengi. Nikichukua miaka 15 kuendelea ukagawia pombe inayotumika Tanzania, kila mtu anakuwa na ndoo ndogo ya pombe nyumbani kwake, na kuwa ndiyo kiwango cha matumizi ya pombe kwa mwaka. Tunamaanisha pombe ambayo ni asilimia 100 ukichanganya unaweza kutengeneza pipa la bia," anasema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wagonjwa wa Kisukari Tanzania (TDA) na Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA), Prof. Andrew Swai, anasema Tanzania imekuwa nchi ya tatu Afrika kwa unywaji wa pombe. "Huko nyuma tulikuwa tunazungumzia Zambia ni walevi, sisi sasa tumekuwa zaidi. Kwa hiyo, pombe siyo nzuri inaharibu ubongo, ini na figo na kumfanya mtu kushindwa kufanya kazi vizuri, inasababisha ajali za barabarani," anasema.

**MADHARA YA POMBE**

Magonjwa yasiyoambukiza kwa sasa yanatajwa kuwa tishio nchini, unywaji pombe kupitiliza na na uvutaji sigara na vileo vingine jamii ya tumbaku vikiwa sehemu ya visababishi vikuu vya maradhi hayo.

Madhalani, kwa ugonjwa wa figo pekee, Tanzania ina wagonjwa karibu 3,000 ambao wana matatizo ya figo kushindwa kufanya kazi na kila mwaka serikali hutumia Sh. bilioni 56 mpaka Sh. bilioni 80, kwa ajili ya kununua vitendanishi ili kuwahudumia.

HABARI KITAIFA

# Othman: Mabadiliko kidemokrasia, kiuchumi, kisiasa haki ya wananchi

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha ACT - Wazalendo, Othman Masoud Othman, amewaeleza vijana kwamba mabadiliko ya kidemokkrasia, kiuchumi na kisiasa na kimaendeleo ndani ya taifa lolote ni haki ya wananchi.

Amesema wananchi ndio wapigakura ili kuamua kiongozi gani ashike madaraka ya uongozi katika nchi yao.

Othman aliyasema hayo juzi katika ukumbi wa Five Star, Kiembe Samaki wilaya ya Magharib 'B' Unguja, alipokuwa akifungua Kongamano la Vijana wa Mkoa wa Mgaharibi B Kichama lililojadili nafasi ya vijana katika kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Kutokana na hali hiyo, Othman aliwataka vijana kufahamu kwamba wao ndio chachu ya mabadiliko hayo yanayohitajika sasa ndani ya Zanzibar katika kuhakikisha inakuwapo Zanzibar mpya yenye uwezo na nafasi ya kupiga hatua zaidi kiuchumi na kimaendeleo kwa kutumia vyema rasilimali za nchi.

Alisema vijana hawana budi kufahamu kuwa hakuna nchi yoyote inayoweza kupiga hatua kiuchumi na kimaendeleo bila kuwa na mamlaka kamili ya kuzitumia ipasavyo rasilimali za ndani zilizoko katika kukuza ajira na maendeleo na kutumia soko la ndani lililopo kwa kuuza biashara ya bidhaa zitakazozalishwa.

Kwa mujibu wa Othman, kazi muhimu ya serikali ni kuwajengea uwezo wananchi hasa vijana kuweza kupata ajira zenye staha na kupata kipato ili kupambana na umasikini jambo ambalo linahitajika sasa Zanzibar kama zilivyoweza kufanya nchi zingine duniani na kupiga hatua kimaendeleo.

Pia aliwataka vijana kutambua kwamba Mapinduzi ya Zanzibar yalilenga kuleta mabadiliko ya kisiasa na kujenga uzalendo kama ilivyofanyika katika nchi mbalimbali duniani kwa vyama vya ukombozi lakini kutokana na kushindwa kutimiza matakwa ya wapigakura vyama hivyo vimeondolewa madarakani na wananchi na kuweka uongozi wanaoamini kwa matumaini ya kimaendeleo.

Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, aliwasisitiza vijana hkuendelea kuandaa makongamano ya namna hiyo ili kuwaelimisha na kufahamu mustakabali wa maendeleo yao na taifa kwa jumla.

Aliewahimiza vijana kuachana na ndoto za kupata uongozi wa udiwani, uwakilishi au ubunge na badala yake fikra zao zilenge katika kuleta mabadiliko ya kweli kwa mustakabali wa taifa.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa ACT- Wazalendo (Bara), Ester Thomas, aliwataka vijana kutokubali kufanywa ngazi ya kupitisha na kuingiza watu kwenye madaraka ambao wataiangamiza nchi na kwamba vijana ndio ukombozi wa nchi.

Akifungua Kongamano hilo, Mwenyekiti wa Vijana Mkoa wa Magharibi Kichama, Malik Juma Mohammed, aliwataka vijana kutobweteka na badala yake wahakikishe wanakuwa na vitambulisho na kuandikishwa kuwa wapigakura kwa kuwa wao ndio wenye jukumu la kuleta mabadiliko ya kidemokrsasia Zanzibar.



Mchungaji Elibariki Nikombolwe (kushoto), akisisitiza jambo kuhusu umuhimu wa malezi bora, wakati wa mkutano wa sikukuu ya vibanda ya siku saba, ulioandaliwa na Kanisa la Waadventista Wasabato la Mbezi, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Viongozi, vijana wasaka fursa kiuchumi

**Na Halfani Chusi**

WADAU wakutana kuweka mikakati ya kutumia fursa za kiuchumi zilizoko jijini Dar es Salaam, ili kuwanufaisha vijana wanaokabiliwa na ukosefu wa ajira.

Walikutanika juzi mkoani hapo kupitia Jukwaa la Maonesho ya Vijana lilikuwa sehemu ya Mradi wa Youth Ready (YR), chini ya mpango wa miaka minne unaoongozwa na World Vision Tanzania na kuungwa mkono na Barrett Family Foundation ya Canada.

Mradi wa YR unalenga kuwawezesha vijana walio nje ya shule kuwa na afya njema, tija na mawakala wa mabadiliko wanaoshiriki kijamii.

Akifungua kongamano hilo lililokutanisha viongozi na vijana zaidi ya 200, Joseph Mhaiki, Mwakilishi kutoka World Vision Tanzania, alisema wamelenga kujadili uvumbuzi wa biashar.

Mhaiki alisema pia, wamelenga kujadili kusoma na kuandika kidijitali na uongozi wa kimataifa, kuhimiza vijana kuchangamkia fursa na kuleta mabadiliko chanya.

Alisema kwa ushirikiano kati ya Asasi ya Umoja wa Mataifa (UNA) Tanzania na Shirika la Afya na Maendeleo ya Wanawake (KIWOHEDE), wanasisitiza dhamira ya kuwawezesha vijana ili kuchochea maendeleo ya taifa.

Alisema katika mpango huo wa YR unaotekelezwa katika Kata za Kivule na Kipunguni wilayani Ilala, Dar es Salaam, una lengo la kuwafikia vijana 1,400 kabla ya kujitanua katika maeneo mengine.

Alisema mpango huo utafanya kazi kwa karibu na washirika mbalimbali ili kuhakikisha kuwa unatekelezwa vyema na kuleta matokeo yaliyokusudiwa kwa kubadilisha fikra na maisha ya vijana.

Ibrahim Mwenda, Mkurugenzi Mtendaji wa UNA Tanzania, alisisitiza umuhimu wa kuongezeka kwa ushirikiano wa ajili ya kuwawezesha vijana.

"Jukwaa hili litasaidia kufungua mawazo ya vijana kwa fursa zinazopatikana kwao," alisema Mwenda.

Mwakilishi Mkazi wa UNDP, Shigeki Kombatsubara, aliwahimiza vijana kutumia zana za kidijitali kwa maendeleo yao.

Mnufaika wa Mpango wa Vijana Kiongozi, Monica John, alisema kuwa mafunzo aliyopata chini ya mpango huo, yamepanua uelewa wake na yametolewa wakati muafaka, ambapo vijana wengi wanakabiliana na changamoto za ajira.

## Watoa huduma za fedha wabanwa mikataba

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

WATOA huduma ndogo za fedha na vikundi vya kijamii vinavyojihusisha na huduma za mikopo vimetakiwa kuwapatia nakala za mikataba wananchi wanaowakopesha mikopo.

Akizungumza katika programu ya elimu ya fedha kwa wananchi wa Mji Mdogo wa Mikumi, Kilosa Mkoani Morogoro, Ofisa Usimamizi wa Fedha kutoka Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Grace Muiyanza, alisema watoa huduma wanatakiwa kutoa mikataba kwa mujibu wa sheria iliyowekwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Muiyanza alisema mkataba ni mafungamano kati ya pande mbili ya mkopeshaji na mkopaji, hivyo ni lazima kila upande uridhie makubaliano hayo kabla ya kuchukua mkopo.

Alisema kwa kufanya hivyo, kutasaidia kupunguza matatizo yanayojitokeza wakati wa kurejesha mkopo na pia mkataba utakuwa njia pekee ya kila mmoja kupata haki itakapotokea migongano baina yao.

Muiyaza aliwasihi wananchi kabla ya kutia saini mkataba wa mkopo ni vizuri kila mmoja akapata nafasi ya kuusoma na kuelewa masharti yaliyomo ili usije ukamfunga kwa vipengele ambavyo vitasababisha ugumu wa kurejesha mkopo.

"Mkataba ni masharti ya pande mbili. Hakikisha umeusoma na kuuelewa mkataba na hata kama ujui kusoma, nenda kwa maofisa wa maendeleo ya jamii wakueleweshe masharti yaliyomo kwenye mkataba huo. Ukiamua kutia saini bila kuuelewa utakuwa umeshakubaliana na masharti na utakuwa umetia saini masharti yatakayokuja kukufunga baadaye," alisema Muiyaza

Awali, akifungua mafunzo hayo, Ofisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mikumi, Edith Mlay, aliwataka wananchi wa Mikumi kuitumia fursa hiyo ya kujifunza masuala ya fedha ili kutatua changamoto mbalimbali wanazokutana nazo kutoka kwa baadhi ya watoa huduma za fedha.

Mlay aliongeza kuwa elimu ya fedha ni muhimu sana kwa wananchi wa Mikumi kwa sababu mji huo umekusanya makundi muhimu ya kijamii yakiwamo ya wakulima na wafugaji.

Alisema elimu hiyo itawasaidia wananchi kutumia fursa za uwekezaji zilizoko katika sekta ya fedha baada ya kuuza mazao yao.

Wizara ya Fedha na washirika wa sekta ya fedha, imehitimisha program maalum ya elimu ya fedha kwa umma kwa mkoa wa Morogoro iliyotolewa katika halmashauri saba ambazo ni Manispaa Morogoro, Wilaya Morogoro, Kilosa, Mvomero, Ifakara, Mlimba na Gairo.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Busara, hekima vinahitajika kwa askari wanapotimiza wajibu wao

**JESHI** la Polisi nchini limepewa dhamana ya kulinda usalama wa raia na mali zao. Nia na madhumuni hasa ni kuhakikisha raia wanaishi kwa amani na usalama bila kupata athari zozote.

Katika kutekeleza hayo yote, jeshi hilo lina idara, vitengo na vikosi mbalimbali vikiwamo vya kutuliza ghasia, kupambana na uhalifu, kufanya upelelezi ili kugundua kama kuna hatari zinazoweza kujitokeza na hatimaye kuchukua hatua madhubuti katika kudhibiti.

Ndiyo maana kumekuwa na habari kutoka katika jeshi hilo kuhusu kuwapo kwa taarifa za kiintelijensia kuhusu hatari ya kuwapo kwa uvunjifu wa amani, hivyo kuchukua hatua za kuzuia mikusanyiko au matembezi ya aina yoyote ili kuzuia kutokea kwa uvunjifu na uharibifu dhidi ya raia na mali zao. Yote hayo ni katika kuhakikisha nchi inakuwa salama na raia wake wanaishi kwa amani na utulivu.

Aidha, ndani ya jeshi hilo kuna kikosi cha usalama barabarani ambacho kazi yake huwa ni kuhakikisha kuna usalama wa kutosha kwa vyombo vya moto na waendeshaji wa magari, pikipiki na waenda kwa miguu wanafuata taratibu na sheria zilizowekwa. Wale wanaokiuka na kuendesha kwa mwendokasi au kutokuzingatia sheria za usalama barabarani huchukuliwa hatua kama kutozwa faini, kupelekwa mahakamani na hata kufungwa gerezani.

Katika kufanya yote hayo kama sheria zinavyotaka, askari wa usalama barabarani, maarufu kama trafiki, wamekuwa wakisimamia masuala hayo na kuchukua hatua dhidi ya wavunjaji wa sheria. Pale wanapohisi dereva anakiuka sheria au chombo cha moto kina kasoro, hukisimamisha na kufanya ukaguzi pamoja na kuomba leseni kwa drereva ili kujiridhisha kama ana kibali cha kuendesha chombo hicho.

Vilevile, askari hao husimamisha magari ya abiria au ya mizigo pale yanapokuwa yamekiuka sheria au kubeba mzigo ama usiostahili au ulio na uzito kuzidi uwezo wa chombo husika.

Pamoja na kutekeleza majukumu yao hayo, zipo kasoro mbalimbali zinazotokana na askari hao barabarani hasa wakati wa kusimamisha magari au kuvuka barabara wakati magari yanapokuwa katika mwendo wa kasi.

Mfano halisi ni katika barabara za Nelson Mandela maeneo ya External na Riverside na Sam Nujoma eneo la Hosteli za Magufuli na Mwenge Vinyago hadi mkabala na kituo cha mafuta cha Oil Com. Katika maeneo hayo imeshuhudiwa askari wa usalama barabarani wakisimamisha magari tena mengine yakiwa kwenye mwendokasi hatua ambayo inaweza kusababisha ajali na kugharimu maisha ya watu.

Wakati wa kufanya hayo, askari hao hujificha pembeni na kuchomoza haraka kusimamisha magari bila tahadhari.

Kuna siku moja basi la abiria linalofanya safari kati ya Tabata Segerea na Kawe lilikuwa katika mwendo mkali kwa kuwa barabara haikuwa na msongamano wa magari. Basi hilo lilipofika hosteli za Magufuli, askari aliibuka na kuliamuru liegeshwe pembeni mwa barabara wakati magari mengine yanakwenda kwa kasi. Jambo hilo lingeweza kusababisha ajali kama dereva asingekuwa makini au kama gari la nyuma lisingepunguza spidi.

Hayo ni miongoni mwa matukio ambayo yamekuwa yakijitokeza katika barabara husasan katika mkoa wa Dar es Salaam kwa askari kutumia mamlaka kufanya hivyo. Lengo hapa si kukosoa utendaji wao wa kazi bali kusihi taratibu za usimamishaji zifuatwe ili kulinda na kuokoa maisha ya abiria na usalama wa vyombo vya usafiri.

Ni wazi kwamba sheria zipo na zinapaswa kufuatwa kama kaulimbiu ya jeshi hilo isemavyo utii wa sheria bila shuruti. Pamoja na kutii huko na polisi kutoa maelekezo kwa madereva kusimamisha magari, ni vyema busara na hekima vikatumika ndiyo maana hata mahakama wakati wa kutoa hukumu zimekuwa zikiombwa kutumia vitu hivyo badala ya kujikita katika vifungu vya adhabu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



## Teknolojia iliyobuniwa na Chuo cha Maji ikomeshe hujuma hii

Na Sabato Kasika

**MAJI** safi na salama ni miongoni mwa mahitaji muhimu ya binadamu yanayopaswa kuzingatiwa kulindwa, kuhifadhiwa na pia kuendelezwa.

Vilevile, huduma bora za maji safi na salama ni sehemu ya haki msingi za binadamu, kwani ni muhimu katika maisha ya viumbe hai, ustawi na maendeleo endelevu ya binadamu katika nyanja mbali mbali za maisha.

Kutokana na umuhimu huo serikali inaendelea kutekeleza kampeni ya kumtua mama ndoo kichwani kwa kusogeza huduma hiyo karibu na wananchi.

Pamoja na juhudi hizo za serikali, kumekuwapo upotevu wa maji kwenye baadhi ya maeneo ya mijini, likiwamo jiji la Dar es Salaam, inawezakana chanzo chake ni ubovu wa miundombinu ya maji kama kuchakaa kwa mipira au mabomba ya maji au hujuma.

Naeleza hivyo kwa kuwa kumekuwapo na taarifa kwamba baadhi hukata mabomba ya wenzao ili wapate huduma hiyo muhimu.

Kitendo cha aina hiyo ni sawa na hujuma, lakini pia hata watu wakikuta bomba limeharibika na kutiririsha maji mitaani, hawatoi taarifa, badala yake inakuwa ni nafuu kwao kwa kupata maji ya bure.

Imekuwa kawaida kutembea hatua chache mitaani na kukuta maji ya bomba yanamwagika barabarani au kukuta watu wanachota maji kwenye bomba lililopasuka.

Wakimaliza kupata huduma hiyo ya bure, wanaacha maji yakiendelea kumwagika bila kutoa taarifa kwa mamlaka husika ili ije kudhibiti upotevu huo wa maji.

Ninaamini kuwa kwa kitendo hicho cha kutokutoa taarifa ni wazi huwa kuna upotevu mkubwa wa maji ambao ungeweza kudhibitiwa iwapo kungekuwa na mwamko wa kutoa taarifa.

> **Nipongeze hatua hiyo kwani kama kweli itafanya kazi, inaweza kusaidia hata kuwanasa wanaohujumu miradi ya maji, hasa wale wanaokimbilia kuchota maji wanaona yanamwagika badala ya kutoa taarifa.**

Lakini wakati kukiwa na tatizo hilo, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso anakuja na habari njema kuhusu teknolojia ya kudhibiti upotevu wa maji mitaani.

Anasema Chuo cha Maji kimekuja na teknolojia hiyo itakayotambua eneo ambalo lina upotevu wa maji ili iwe rahisi kulifuatilia haraka.

Nipongeze hatua hiyo kwani kama kweli itafanya kazi, inaweza kusaidia hata kuwanasa wanaohujumu miradi ya maji, hasa wale wanaokimbilia kuchota maji wanaoona yanamwagika badala ya kutoa taarifa.

Kwa kuwa kuna habari njema kwamba Chuo cha Maji kimekuja na teknolojia ya kutambua upotevu wa maji kwenye miundombinu ya maji, ni vyema wale waliozoea kufanya hujuma wajue kuwa hawana ujanja tena.

Inaelezwa kuwa teknolojia hiyo ya kisasa inatambua maeneo ambayo yana upotevu wa maji katika miundombinu ya maji ili kuwezesha utatuzi wa haraka wa tatizo hilo.

Kwa mujibu wa waziri mwenye dhamana ya maji, teknolojia hiyo imeanza kutumika kwenye baadhi ya maeneo na imeonyesha ufanisi.

Labda nimtonye waziri kuwa mara nyingi maeneo yenye tatizo hilo, mengi ni ya uswahilini ambalo unakuta watu wanachimba ya mipira ya ya wenzao na kuikata na kukinga maji.

Maeneo hayo yangemulikwa na teknolojia hiyo haraka ili kukomesha vitendo hivyo vya hujuma vinavyosababisha wengine kukosa huduma ya maji.

## MAKALA

**FIKRA MBADALA**

# Kila Mtanzania aone fahari kulipa kodi



Pascal Mayalla

WIKI hii, kulifanyika kikao kazi kati ya Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuhusu namna ya kuwatumia wahariri, waandishi wa habari na vyombo rasmi vya habari kueneza elimu ya kodi. Lengo mahususi la kufanya hivyo ilikuwa kuwaelimisha walipakodi umuhimu wa kulipa kodi na wajisikie fahari kufanya hivyo.

Kutokana na fursa hiyo, Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, aliipongeza TRA kwa kuwashirikisha wahariri na vyombo vya habari katika suala zima la utoaji wa elimu kwa walipakodi, badala ya jukumu hilo kubebwa na TRA wenyewe.

Balile alisema kama TRA itawatumia kikamilifu wahariri na vyombo vya habari kuelimisha umma kuhusiana na mambo ya kodi, kutakuwa na mafanikio makubwa kwa kuwa vyombo hivyo vinawafikia wananchi wote. Kwa mantiki hiyo, wananchi wakielimishwa kuhusu kodi na matokeo ya kodi zao, watakuwa wanalipa na kujisikia fahari.

Balile alitolea mfano mkoa wa Iringa kwamba hakuna purukushani za kulipa kodi wala kukimbizana na wafanyabishara kuhusu jambo hilo. Sababu kubwa ni kwamba kitengo cha elimu kwa mlipakodi mkoani humo kimekuwa kikitoa elimu wananchi kupitia vyombo vya habari vya Iringa, zikiwemo redio za jamii. Kutokana na hali hiyo, walipakodi wa Iringa wameelewa umuhimu wa kodi, wanalipa kodi bila shuruti na hakuna kukimbizana wala kamatakamata au fungia fungia biashara kati ya wafanyabiashara na TRA.

Balile alimpongeza Mkuu wa Kitengo cha Elimu kwa Walipakodi wa Iringa, Paul Walalaze, kwa ushirikiano wake na vyombo vya habari vya Iringa. Kwa sasa Walalaze amehamishiwa makao makuu ya TRA kuwa meneja wa elimu kwa walipakodi, hivyo Balile amkataka kukifanya kile alichokifanya Iringa kwa Tanzania nzima, walipakodi waelimishwe kuhusu kodi, TRA wadai kodi halali na watu walipe kodi bila shuruti.

Kwa upande wake, Walalaze akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Elimu kwa Mlipakodi, Richard Kayombo, alisema kwa kutambua umuhimu wa vyombo vya habari katika kuyafikia makundi yote ya jamii, TRA imeamua kushirikiana na TEF kama wadau muhimu wa kufikisha elimu ya kodi kwa wananchi.

Walalaze alisema kuanzia mwaka huu wa fedha, TRA katika mikoa yote itazitumia redio za jamii kueneza elimu ya kodi na wahariri wakashauri si tu itumie redio za jamii pekee bali pia televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii kila mkoa.

Kwa kuanzia TRA inaanzisha kampeni ya "Hakiki Stempu", kutumia vyombo vya habari kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuhakiki Stempu za Kielectroniki (Electronic Tax Stamp - ETF) kwenye bidhaa mbalimbali za vinjwaji, zikiwamo maji, bia, soda, mvinyo na vinywaji vikali vyote vinavyozalishwa nchini na vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi.

Wananchi wakielimishwa kuhakiki stempu hizo, si tu watabaini kama bidhaa hiyo ni halali bali itawasaidia kubaini bidhaa bandia, hivyo kusaidia kulinda afya za watumiaji. Kwa maana hiyo, ukigundua ni bidhaa bandia, usinywe kinywaji hicho kwa usalama wa afya yako.

Mjumbe wa kamati ya uongozi ya TEF, Salim Said Salim, kutoka Zanzibar, ambaye ni mmoja wa waandishi wa habari wakongwe nchini anayeandika mpaka sasa huku akielekea umri wa miaka 80, aliishauri TRA kuwa wananchi hawapendi kuona wananchi wa kawaida ni masikini wa kutupa, wanaoishi kwenye lindi la umasikini uliotopea, lakini bado wanakamuliwa kodi, halafu TRA inatoa misamaha ya kodi kwa matajiri! Alishauri misamaha ya kodi isiwapo bali kila mtu alipe kodi.

Pia Salim alizungumzia adhabu kali kwa wakepaji wa kodi, halafu adhabu kiduchu kwa wezi wa mali ya umma, wahujumu na wala rushwa, hivyo akataka wapewe adhabu kali kabisa kama wahalifu hatari.

Mafundisho yote ya dini yanafundisha kuwa: "Mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari na mpeni Mungu yaliyo ya Kimungu". Lengo la mafundhisho hayo ni kuwathibitishia waumini wote wa dini zote kuwa tawala zozote zilizo madarakani kwa mujibu wa sheria, zinapaswa kuheshimiwa, kuungwa mkono na kupewa utii wa sheria bila shuruti, taratibu na kanuni. Miongoni kwa mwa hayo ya Kaisari ni pamoja na kulipa kodi. Watu wote lazima walipe kodi ili kuiwezesha serikali kuendesha nchi, hivyo vitendo vyovyote vya ukwepaji kodi wa aina yoyote si tu ni ukiukwaji wa sheria, bali pia ni dhambi mbele ya Mwenyeezi Mungu.

Katika sheria zetu za kodi, tuna sheria mbili. Moja ni sheria ya watu wengine wote kulazimika kulipa kodi na nyingine imewatenga baadhi ya viongozi fulani fulani kwa kuwapa msamaha wa kutokulipa kodi yoyote kwa mujibu wa sheria.

Wahariri wanapendekeza kuondoa hiyo 'double standards' ya kodi kwa wananchi kutozwa kodi, huku baadhi ya viongozi wakisamehewa kulipa kodi. Hali hiyo inawafanya wasilipe kodi. Hatua hii pia inawafanya viongozi wasiyaishi maisha wanayoyahubiri. Haiwezekani kiongozi ahamashishe kila mtu alipe kodi huku kumbe yeye mwenyewe halipi kodi.

Hii ni sawa na kasisi mtenda dhambi kuhubiri watu waache dhambi ilhali yeye anatenda! Badala ya kuwa mfano, anawaambia waumini wake kwamba wayafuate maneno yake na si matendo yake!

Ni dhahiri kwa hili likifanyika, litaondoa 'double standards' katika masuala ya ulipaji kodi. Kila mtu kulipa kodi, tena baadhi ya wahariri wameshauri, 'Tax Clearance certificate' ya TRA iwe miongoni mwa sifa za kugombea uongozi ili tupate viongozi waadilifu.

**Mungu Ibariki Tanzania.**
**Paskali**
**+255 754 270403**

# Wanufaika TASAF wagombea bima ya afya

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WANUFAIKA wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaoendeshwa na Mfumo wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika vijiji vya Nanjoka, National Housing na Nakayaya wilayani Tunduru, wamegoma kuchangia bima ya afya.

Kwa mujibu wa wanufaika hao, wameamua kufanya hivyo kwa sababu wanakosa matibabu pindi wanapokwenda hospitalini.

Waliyabainisha hayo kwa nyakati tofauti wakati Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Simon Chacha, alipofanya uhamasishaji wa kujiunga na bima ya afya. Mbali na kuwaongezea fedha endapo watakubali kuchangia kiasi kidogo cha fedha kwa lengo hilo lakini hawakukubali.

Kilichowakatisha tamaa ya kuendelea kuchangia huduma hiyo, kwa mujibu wa Fikira Buji na Huruma Dugange ni kwamba mwaka 2022/23 maofisa wa TASAF waliwashawishi na kuwakata fedha zao kwa ajili ya huduma hiyo.

Walisema walipougua walipatwa na jambo ambalo hawatalisahau. Walisema walichojifunza ni kwamba huduma ya bima inachagua magonjwa na mgonjwa mwenye bima akifika hospitalini anapuuzwa. Pia walisema mgonjwa mwenye bima ukienda hospitalini huishia kupata huduma ya maandishi ya mganga na kuelezwa dawa ukanunue kwenye duka la kutoa huduma hiyo.

Hata hivyo, Chacha alisema pamoja na mambo mengine, aliwataka wanufaika hao kuridhia mpango huo kama sehemu ya kujihakikishia upatikanaji wa huduma za matibabu pindi watakapougua.

"Nani yupo tayari kuchangia hata kwa kutoa kiasi kidogo cha fedha mimi nitamwongezea," alisema Chacha wakati wa uhamasishaji na kumpata Zainabu Mayanga pekee ambaye alimlipia Sh. 25,000 baada ya kutoa Sh. 6,000.

Pamoja na ushawishi wake kugonga mwamba, Chacha aliendelea kuwahimiza wanufaika hao kuona umuhimu wa kujiunga na kuchangia bima ya afya ili kujihakikishia matibabu pindi watakapougua.

Akizungumzia msaada huo, Zainabu alisema aliamua kutumia nafasi hiyo kutokana na afya yake kuwa na mgogoro kwa kuwa amekuwa akiugua mara kwa mara.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Tunduru, Muhidin Shaibu, pamoja na kukiri kukutana na kero hiyo kuwa iko maeneo mengi kipindi cha uhamasishaji, alisema suala la bima ya afya ni muhimu vkwa wanufaika hao ili kuwa na uhakika wa matibabu baada ya kuugua.

Aidha, Shaibu aliahidi kupeleka malalamiko hayo kwa viongozi wanaosimamia huduma hiyo ili wafanye ufuatiliaji na kutafuta mbinu ya kurekebisha kero hiyo.

# Miradi ya nishati kunufaisha wananchi wa maeneo iliyomo



**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wanaoishi katika maeneo ambayo yana miradi mikubwa ya nishati watanufaika kupitia upatikanaji wa huduma mbalimbali.

Naibu Waziri wa Nishati, Judithi Kapinga (pichani), alisema hayo juzi bungeni jijini Dodoma alipokuwa akijibu swali la Ally Kasinge (Kilwa Kusini - CCM).

Mbunge huyo alitaka kujua mkakati wa serikali katika kuhakikisha Kisiwa cha Songosongo mkoani Lindi ambako kuna visima vya gesi asilia na mitambo ya kuchakata gesi kinapata umeme wa uhakika.

"Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alishatoa maelekezo kuhakikisha wananchi hawa si tu wanapata umeme wa uhakika bali na huduma zingine za kijamii ziimarishwa," alisema.

Naibu Waziri aliliuhakikisha bunge kuwa, tayari serikali imeanza kulifanyia kazi agizo hilo kwa kuhakikisha wananchi wa Songosongo wanapata umeme wa uhakika na huduma za kijamii ambazo zinaendana na miradi iliyoko katika maeneo yao.

Akizungumzia upelekaji umeme wa gridi kwenye maeneo ya visiwa, Kapinga alisema Tanzania ina visiwa takriban 120 na serikali imeanza kufanya tathmini ya kufikisha umeme wa gridi katika maeneo hayo.Kapinga aliongeza kuwa kwa sasa visiwa hivyo vinatumia umeme wa jua na kwamba serika imeweka ruzuku ya asilimia 50 hadi 55 ili wananchi wapate umeme wa uhakika kwa muda wote.

# HABARI PICHANI



Moja ya majengo ya Shule ya Msingi Kamatondo, katika Kijiji cha Kamatondo, wilayani Musoma, mkoani Mara, likiwa limeezuliwa mabati kutokana na mvua kubwa ya upepo iliyonyesha juzi na kuezua madarasa mawili na ofisi ya walimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto la Polisi Wilaya ya Mbozi, mkoani Songwe, Mkaguzi wa Polisi, Sada Salum akitoa elimu ya madhara ya ukatili na matumizi mabaya ya mitandao kwa wanafunzi wa Kidato cha tano wa Shule ya Sekondari Vwawa Day, mwishoni mwa wiki. **PICHA: ISSA MWADANGALA**



Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Dorothy Semu akimvisha kofia mwanachama mpya kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Edmund Nditi, aliyejiunga na chama hicho, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki**. PICHA: JOHN BADI**




Raia wa Marekani, Brandon Dashaurn, akiwa chini ya ulinzi wa askari magereza, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam juzi, baada ya kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 jela kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya aina ya Mescaline gramu 54.04. **PICHA: IMANI NATHANIEL**



Wakazi wa mji wa Kondoa, mkoani Dodoma, wakifanya usafi wa kutoa mawe kwenye mtaro wa maji ya mvua, mwishoni mwa wiki.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# MAISHA

SEPTEMBA 1, 2024
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
*Jumapili*

Ukurasa 14

## NGOZI LAINI BILA VIPODOZI



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Tengeneza nyumba maalum ya kufugia mbwa nyumbani



Ukurasa 12

## HARUSI





# SWEATPANT NI BALAAA

Ukurasa 13

## WATOTO

### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| C | ■ | C | H | A | M | A |
| H | ■ | ■ | ■ | D | ■ | S |
| A | ■ | T | U | A | ■ | T |
| G | U | U | ■ | B | A | A |
| U | ■ | M | B | U | ■ | A |
| Z | ■ | B | ■ | ■ | ■ | F |
| I | B | A | K | I | ■ | U |


### FUMBO TOTO

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ■ | | | | | |
| | ■ | ■ | ■ | | ■ | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | | | ■ | | | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | ■ | | ■ | ■ | ■ | |
| | | | | | ■ | |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

BUU, NAE, WAO SAA, SWALA, UJAZO, AGUSE, BONDA, THAWABU, ASTAAFU

### TOA TOFAUTI 5




## PAKA RANGI



### AMSHA AKILI

HAYA WATOTO WAZURI, WEKA KIVULI KWENYE KILA NUKTA ILI UJUE NI NANI AMEFICHWA KATIKA MAUMBO HAYA.



### CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma na rafiki yake John walikuwa wakitembea pembeni ya barabara wakielekea shambani. Wakati wakikaribia shambani, Juma alimuona ndege akipaa angani huku akiyumbayumba kwa madaha.Juma alifurahi sana na kuanza kumuuliza rafiki yake.

**Juma:** Ona yule ndege anaruka kwa furaha

**John:** Nimefurahi baba kasema ukimuona ndege ana furaha atakuwa na makinda.

**Juma:** Kwani ndege sawa na mnazi una makinda?

**John:** Hapana ila watoto wa ndege wanaitwa makinda na sio mnazi.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Unachomtenda mwenzako nawe utatendwa

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na vitimbwi vya safu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki iliyopita nilimwelezea dada mmoja aliyenidokeza kwamba alijua yeye ni bi-mdogo peke yake kumbe yuko mwingine!

Ukiona unaoa wake wengi au mwanamke unaolewa na mwanamume mwenye wake wengi, jua kuwa iko roho chafu ya mitala inayofanya kazi. Ni roho inayosababisha mambo mengi kuwatokea wanandoa.

Hii roho husababisha kukosekana kwa upendo kati ya wanandoa, kutofurahia ndoa, ugomvi usioisha. Pia imesababisha hatma za watu wengi kuharibika. Ni chanzo cha ndoa nyingi kuvunjika, kuoa na kuacha na kuwafanya watu wawe wajane katika umri mdogo.

Makala iliyopita nilitoa mfano wa mwanamume ameoa mke wa kwanza ambaye anaishi naye. Lakini akatafuta mke wa kando akamweka kinyumba na kumzalisha watoto. Tena akaoa mwingine akamweka kinyumba na kumzalisha watoto. Hii ni roho kamili ya mitala.

Kuna msemo kwamba adui wa mtu ni mtu. Anaweza kuwa ndugu yako, rafiki au watu wa familia yako uliowaamini lakini wakakugeuka. Unakuwa kwenye nafasi yako ukadhani uko salama kumbe yuko adui anainyemelea hiyo nafasi yako. Iwe ni nyumbani (ndoa) au kazini, ofisini hata kwenye biashara.

> **“Wanaotafuta nafasi ni wengi na wengine wana sifa kuliko waliopo kwenye nafasi nzuri. Mtu mwenye tabia mbaya hana mtetezi, hasa wale wenye tabia zisizobadilika.**

Lakini kumbuka ukimtoa mtu kwenye nafasi yake kibabe, uwezekano ni mkubwa sana kwa wewe pia kutolewa kwenye hiyo nafasi. Wanawake wengi wanatolewa kwenye nafasi zao muhimu kutokana na roho ya uchawi.

Uchawi ni silaha kubwa ambayo shetani anaitumia ili kuwaangamiza wanadamu. Uchawi ni silaha ya uharibifu inayotoka kuzimu ikiwa na lengo la kuua na kuangamiza wanadamu. Ni nguvu ya kufanya uovu na uharibifu. Ni roho inayopindisha hatima ya mtu. Ni roho inayomkandamiza na kumtawala mtu.

Wanawake wengi huitumia sana uchawi katika kulazimisha uhusiano. Wako wanaokwenda kwa waganga wa kienyeji ili kupata dawa za kuchawi kumdhibiti mwanaume ili aolewe naye. Wanaume wengi wamejikuta wakioa wanawake ambao kabla waliwapumbaza ufahamu na kuwaoa kirahisi pasipo kujua.

Hawa ndio nawajadili hapa leo na si wale ambao Mungu amewaunganisha na kuwapa ndoa na familia nzuri isiyo na misukosuko, ambao ni wacha Mungu waliosimama katika imani ya kweli.

Endapo mke wa kwanza aliingia kwenye ndoa kishirikina, ni dhahiri atatokea mwingine baada yake. Huyu naye asishangae kujikuta yupo mwingine kwani hiyo ni roho kamili ya mitala iliyochanganyika wakati mwingine na roho ya uchawi.

Ni kanuni ukiiba nawe ipo siku utaibiwa. Na wale wanaotumia dawa za kichawi wanajua fika kwamba huwa zinachuja (isha nguvu), na hapo mwanaume akili hurudi. Sasa akinaswa na mtego wa kichawi wa mwanamke mwingine huko utafanya nini?

Naye huyu atawekwa kinyumba kama mke wa pili pembezoni. Atatunzwa lakini mwanaume hataacha kutafuta mwingine hasa kama ana uwezo kifedha kama ilivyotokea kwa dada niliyemwelezea wiki iliyopita.

Awali nimesema kuwa adui wa mtu ni mtu. Tambua kuwa una maadui wengi, tusiishi kama vile hatuna maadui. Kukosa kujua kuwa una maadui ni kosa la kukupelekea kifo. Kila mtu mwenye kitu lazima awe na maadui, ni lazima awe na maadui iwe anajua au hajui.

Mungu mwenyewe anao maadui kama neno lake linavyothibitisha; “Mungu huondoka, adui zake wakatawanyika, nao wamchukiao huukimbia uso wake. (Zaburi 68:1). Si kila anayecheka nawe ni mwema kwako. Mwingine yupo karibu ili kuzijua siri za nguvu zako!

Wengi wamepoteza nafasi zao nzuri kwa kuwa wamemwacha Mungu na kutegemea nguvu za shetani (ushirikina). Kumbuka tabia yako mbaya inaweza kuwa mlango wa mtu mwingine kupewa nafasi yako.

Wanaotafuta nafasi ni wengi na wengine wana sifa kuliko waliopo kwenye nafasi nzuri. Mtu mwenye tabia mbaya hana mtetezi, hasa wale wenye tabia zisizobadilika.

Fahamu chanzo cha mafanikio yako na ukilinde. Mtu mwenye akili hulinda chanzo cha mafanikio yake. Kila mafanikio au nafasi uliopo ina chanzo. Haikutokea tu bali kipo kilichosababisha wewe kuwepo kwenye nafasi hiyo.

Tatizo ni kwamba wengi hawajui kilichowafanya kuipata nafasi fulani. Na wakati mwingine hata wakijua, wao wenyewe huwa ndio chanzo cha kupoteza. Kumbuka, ukimtenda mwenzako baya utarudishiwa baya. Maisha ndivyo Yalivyo!

***Je, una maoni, ushauri? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi

# Mwambieni ni suala la muda atunze kumbukumbu

SIASA inahitaji kumbukumbu na kutunza kumbukumbu. Ndiyo, siasa inahitaji angalizo na kuweka angalizo. Bila shaka utakubaliana na mimi kwamba siasa inahitaji utafiti.

Godbless Lema, Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Mbunge wa zamani wa Arusha, anapaswa kutunza kumbukumbu ya unabii wake.

Karibu kila wakati anazungumza juu ya siasa za ulinganisho, lakini siku mbili zilizopita, alikuja na maono yake dhidi ya mpira wa Tanzania.

Sawa ni mawazo yake. Katika mitandao ya kijamii amepigwa mawe kutokana na kauli yake kuhusu mpira wa Tanzania. Sina tatizo na hilo, ila nataka aweke kumbukumbu sawa kuhusu siasa za ulinganisho anazozifanya.

Siasa za ulinganishi, yaani ‘comparative politics’ ndio aina ya siasa inayofikirisha zaidi na kuvuta hisia za wengi.

Linganisha masuala ya uchumi, kuongezeka kwa makali ya gharama za maisha, mahitaji ya ajira, kipato duni au kupaa kwa bei ya bidhaa mbalimbali kunakotokana na mfumuko wa bei, utaziona sura tofauti za Watanzania.

Ulinganisho wa kushughulikia vitu badala ya watu, ndiyo ajenda kubwa inayohusu siasa za ulinganisho.

Watanzania wanaokaa katikati ya nchi huko bara, wanaweza wasielewe masuala ya utawala tofauti na watu wa pembezoni.

Kwa mfano, uchumi mkubwa wa Kilimanjaro, unategemea kitu kinachoitwa kwa kiingereza ‘remittance’. ‘Remittance’ ni fedha wanazotegemea wakazi wa Kilimanjaro, kutumwa na watoto, au ndugu walioko mbali na Kilimanjaro.

Natamani wanasiasa wetu wakosoane kwa hoja za siasa za ulinganisho ili kuja na mwarobaini matatizo ya wananchi.

Mathalani, wanaweza kukosoana ili kutafuta suluhu ya muda mrefu ya vijana wengi kupoteza matuimaini ya maisha.

Vijana wengi wanakata tamaa kwa sababu hakuna kazi, wakiamka asubuhi hakuna kiwanda wanachokwenda kufanya kazi.

Matokeo yake tunayoyashuhudia leo, ni namna wanavyojipongeza kwa pombe kali na hatarishi kwa afya zao, ili tu kupunguza msongo wa mawazo.

Katika siku za usoni, nimeguswa na aina ya siasa za ulinganisho zinazofanywa na baadhi ya wanasiasa nchini, hasa Godbless Lema, akifanya ulinganisho wa vitu au bidhaa. Lema anasema Tanzania wananunua maziwa kila mwaka ya thamani ya Sh. bilioni 34.5 kutoka nje ya nchi.

Anasema: “Nyie mkipewa ng’ombe wanaozalisha maziwa kwa wingi, mkatengenezewa mashamba ya kuzalisha vyakula vya ng’ombe, hamuwezi kufunga ng’ombe nyie?

“Mahindi pamoja na wakulima wa Tanzania kulima, serikali wanaleta ya bilioni 64, sukari Sh. bilioni 265, mchele tutunanua kila mwaka Sh. bilioni 146, maharage ya soya Sh. bilioni 34, njano Sh. bilioni 554 na mafuta ya kula Sh. bilioni 694.Jumla yake karibu trilioni mbili. Vyakula vyote hivi, bidhaa zote hizi zinaweza kulimwa Mkoa wa Manyara peke yake.

Yaani maana yake, Sh. trilioni mbili ikibaki Manyara kila mwaka kwenye mazao huku tusingeona lami za kubabaisha. Kungekuwa na lami, kungekuwa na vyuo, watoto wangesoma na watu wangekuwa na maisha bora.

Uchumi ni maarifa ndiyo maana Abu Dhabi (makao makuu ya Umoja wa Falme za Kiarabu-UAE) ni jangwa lakini wana uchumi mzuri kuliko Tanzania.

Lema anasema: “Hanang’ kuna shamba la ngano, yale mashamba yamekufa. Leo tunaagiza ngano ya Sh. bilioni 500 kutoka Ukraine.”

Lema anaenda mbali zaidi akisema. Jiulize Sh. bilioni 500 ingekuwa inabaki Hanang’ kila mwaka Hanang’ ingekuwa kubwa kuliko Dar es Salaam. Kahawa imesomesha vijana wote wa Kichaga. Kahawa imesomesha vijana wote wa Kagera, kahawa ni zao la pili duniani, baada ya mafuta kwa kuuzika.

“Kahawa leo imekufa Kilimanjaro, kahawa imekufa Kagera, kahawa imekufa kila mahali. Hata yale mazao yanayoota bila mbolea nchi hii imeshindwa kuyasimamia,” anasisitiza.

Tukosoane kwa hoja, tufanye siasa za ulinganisho, sio kueleza nasaba ya mtu. Hakuna jambo litakaloijenga nchi yetu kama kukubaliana kutokubaliana katika hoja.

Tuvumiliane, tukosoane kwa staha katika siasa za ulinganisho, maana tunajenga nyumba moja.

• ***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI











Ilikuwa siku ya furaha kwa wazazi wa Zulfa Hassan Hussein baada ya kuandaa sherehe ya kumuaga binti yao ambaye amefunga ndoa na Hussein Juma Hassan Agosti 23, mwaka huu nyumbani kwa bi harusi Yombo Vituka, jijini Dar es Salaam ambayo pia ilihudhuriwa na Mama Siti Mwinyi.

MITINDO

# SWEATPANT NI BALAAA

VAZI la 'Sweatpant' ni aina ya suruali laini ambayo inampa mtu uhuru wa kufanya shughuli mbalimbali bila kupoteza mwonekano wake halisi.

Suruali za aina hizi hazina ukakasi kama mtu akivaa akiwa chumbani, sebuleni, ukumbi wa mazoezi au maongezi na marafiki .

Ukweli ni kwamba ukiwa umevaa Sweatpants utakuwa umejipa uhuru wa ziada wa kufanya mambo mengi kwa wakati mmoja.

Hata hivyo, ni vyema ukawa mbunifu katika matumizi ya suruali hizi katika kila mazingira, mfano unapokuwa mazoezini hakikisha juu unavaa fulana laini na yenye uwezo wa kupitisha hewa.

Ukiwa matembezini, sebuleni au kukutana na rafiki zako hakikisha suruali yako inaambatana na nguo nzito kiasi kama fulana ya pamba ambayo itakuweka katika hali ya utulivu kwenye ukumbi.

Ujanja wa kutengeneza mwonekano bora zaidi utakuwa juu yako, kwani unaweza kuongeza kwa kuvaa viatu vya raba nyeupe au sando ukatoka bomba zaidi.





UREMBO



# NGOZI LAINI BILA VIPODOZI

NI wazi kila mwanamke anapenda kuwa na ngozi lakini mwororo na inayovutia kwa kutizama na kushika.

Mbali na kutumia vipodozi vya kung'arisha ngozi, yapo mambo ya muhimu ya kuzingatia yanayosaidia ngozi yako kuwa nyororo.

**ZINGATIA MLO WAKO**

Hakikisha unakunywa maji si chini ya glasi nane kwa siku na matunda pamoja na mboga kila unapopata mlo.

Matunda na mboga za matawi husaidia oksijeni kuzunguka vizuri mwilini na kwenye ngozi kuliko mafuta au kipodozi chochote unachoweza kupaka.

Protini husaidia kujenga ulinzi zaidi katika seli za ngozi ambayo ngozi inahitaji kukabiliana na ukavu wa ngozi.

**USAFI KWANZA**

Osha uso wako kila mara. Watu wengi hukimbilia kuosha nyuso zao harakaharaka kwa sababu kuna uwezekano mkubwa wa uchafu kubaki, hasa wanawake ambao wanatakiwa kutambua umuhimu wa uso zao.

Basi ni bora ukatenga muda wa kutosha katika kuosha na kutunza uso.

Kusafisha uso mara mbili kwa siku ni vizuri kwa utunzaji wa ngozi yako ya uso.

Baada ya kufanya hivyo ni muhimu upake mafuta kiasi. Mafuta ni kwaajili ya kulainisha na kung'arisha ngozi. Hata ijapokuwa una ngozi ya mafuta mengi, ni vizuri kutafuta mafuta ya ngozi.

**TUNZA MACHO YAKO**

Watu wengi hupaka kiasi kidogo cha mafuta chini ya macho bila kujua faida tunazoziacha kwa kutokufanya hivyo.

Kuna mistari au mikunjo inaanzia kwenye jicho na ambayo muda mwingine husogea hadi kwenye maeneo ya karibu na nywele unatakiwa upake mafuta ili kuondoa uzee.

**BARAFU**

Barafu ni moja kati ya vitu muhimu katika kutunza ngozi. Licha ya upatikanaji rahisi pia ina uwezo wa kutunza ngozi yako bila gharama.

Faida za kutumia barafu katika utunzaji wa ngozi yako ni kwamba; Ukiumia au kujichuna kwenye ngozi waweza kutumia barafu kupunguza wekundu na kupunguza mwasho katika eneo lile.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Kaanga karanga kwa Microwave

INAWEZEKANA umezoea kutumia microwave kupasha chakula na vinywaji kama chai au kahawa. Leo nitakupa moja ya maujanja ambayo unaweza ukayafanya kwa kutumia kifaa hicho kinachotumia umeme.

Unachotakiwa kufanya ni kununua karanga mbichi, hazina gharama sana na si lazima ukaange kilo nzima kwa siku moja, unaweza ukakaanga robo na nyingine ukatumia siku nyingine.

Mahitaji

Uandaaji wa karanga hauna mambo mengi, vitu muhimu vinavyohitajika ni chumvi, maji, pamoja na sahani ambayo inahimili joto la microwave hadi karanga zitakapoiva.

Jinsi ya kupika



Hatua ya kwanza, chambua karanga zako kutoa maganda na karanga zingine ambazo zinaweza kuwa zimeoza au kuharibika, Kisha chukua karanga na uziweke kwenye chombo ambacho utakitumia kwenye microwave.

Baada ya hapo, chukua maji kidogo na chumvi kiasi upendacho na uvikoroge kwenye kikombe. Chumvi ikiyeyuka, chukua mchangayiko huo na unyunyize kwenye chombo chenye karanga, kisha changanya ili karanga zipate chumvi vizuri.

Hatua inayofuata ni kuziweka karanga kwenye microwave, kwenye hatua hii hakikisha huweki muda mrefu ili karanga zisiungue.

Kwa kawaida inaweza kuchukua dakika tano za joto la wastani hadi karanga kuiva.

Unachotakiwa kufanya ni kuweka muda wa dakika mbili mara ya kwanza, zikiisha angalia karanga zina hali gani. Namaanisha uonje na uchanganye.

Kama hazijaiva, weka tena dakika mbili, nazo zikipita onja kama karanga zimeiva vile unataka.

Unaweza kula karanga zako na juisi, chai au kinywaji unachopendelea.



## MAISHA NI NYUMBA
Na Restuta James

# Tengeneza msitu nyumbani

WATAALAMU wa mapambo ya ndani wanaeleza kuwa uwepo wa miti mbalimbali nyumbani unaweza kutengeneza madhari mujarabu ya kukuongezea utulivu na kuondoa msongo wa mawazo uwapo nyumbani.

Wanaeleza kuwa ni suala la kuamua na kuanza kutengeneza madhari hiyo ya kuvutia kwa kupanda miti tofauti tofauti, mikubwa kwa midogo ili kupata msitu unaoutaka.

Mtaalamu Bahati Boaz, anasema iko miti isiyokua haraka inayoweza kupandwa kwenye makopo makubwa ya maua na kuwekwa kibarazani au chini kwa mpangilio unaoutaka.

Anasema ipo inayostawi vizuri kama ikipata kivuli na ipo inayohitaji jua na mwanga zaidi; na kushauri kuwa kabla ya kuanza kutengeneza msitu nyumbani kwako, fahamu vyema miti na maua unayoihitaji.


Anapendekeza kuwa miti mizuri ni ya matunda kama michungwa, miembe na minazi kulingana na ukubwa wa eneo lako, kwa kuwa inaweza kuwa na faida zaidi, lakini miti mingine nayo inahitajika ili kukamilisha dhumuni la kuwa na mazingira ya asili nyumbani.

Anasema tafiti nyingi zimethibitisha namna ambavyo miti inaweza kusafisha hewa japokuwa ni muhimu kuzingatia kupanda ile isiyohatarisha nyumba au kuvutia wadudu wakali kama ng'e, tandu na nyoka.

Baadhi ya miti inayopendekezwa kupandwa ni parlor palm unaotajwa kusafisha sana hewa na wenye uwezo wa kutengeneza msitu haraka.

Mwingine ni yucca cane ambao unaweza kuupanda karibu na mti mwingine kwa kuwa unastawi vizuri ukiwa kwenye kivuli, japokuwa hauhitaji maji mengi.

Anashauri kwamba chini ya miti kupandwe maua ili kutengeneza mazingira asilia.



# Tengeneza nyumba maalum ya kufugia mbwa nyumbani

NYUMBA ni moja ya mambo muhimu sana katika maisha ya binadamu. Iwe ni ya kupanga au ya kumiliki mwenyewe. Ndiyo maana kumekuwa na msemo kwamba maisha ni nyumba. Yote hiyo ni kuonesha umuhimu wa nyumba kwa maisha ya kila siku ya mwanadamu.

Kutokana na umuhimu wa nyumba na ili iendelee kustawi kwa kuwa msaada zaidi, inahitaji kujengwa kwa viwango bora ili isiharibike haraka na iwe rafiki wa mazingira.

Kwa mantiki hiyo, nyumba inahitaji matunzo ikiwamo kufanyiwa usafi na kukarabatiwa pale inapohitajika kufanyiwa hivyo.

Kama ilivyo katika ujenzi bora kwa nyumba ya binadamu, kadhalika na kwa wanyama. Nao baadhi wanahitaji kuishi katika nyumba ili kulinda ustawi wao. Mtaalam wa kufuga mbwa, Richard Chacha, anasema mbwa wanaofugwa kwa ubora wanatakiwa kufugiwa katika nyumba maalum.

Anasema nyumba ya mbwa mara nyingi inatakiwa iwe ndani ya uzio wa nyumba ya mfugaji mwenyewe kwa sababu pia anahitaji uangalizi na kuepusha hatari ya kudhuru watu.

"Ufugaji wa mbwa ni jambo jema kwa sababu lengo lake ni kuimarisha ulinzi katika nyumba, badala ya kutumia au kuajiri walinzi katika suala la usalama. Ukiwa umefuga mbwa inasaidia zaidi na huyu ana faida nyingine kwa sababu akiwa ni mbwa ambaye amefugwa vizuri na kufundishwa, ni rahisi kubaini wahalifu kwa sababu mbali na kupambana nao lakini hutoa kelele za tahadhari,"anasema Chacha.

Anasema ili ufurahie kuwa na mbwa bora, lazima pia umjengee makazi bora ili awe na afya njema.

Chacha anasema baadhi ya vitu muhimu ambavyo unapaswa kuzingatia wakati wa ujenzi wa nyumba ya mbwa ni pamoja na kuhakikisha inakuwa na nafasi ya kutosha ambayo itamwezesha kujigeuza kwa kadri anavyohitaji.

Anasema nyumba ya mbwa inapaswa kuezekwa kama kawaida japokuwa siyo lazima iwe bati. Pia anasema lazima iwe na mwanga wa kutosha badala ya giza ili kumwezesha kufanya shughuli zake za ndani kwa ndani.

Jambo lingine anasema lazima uhakikishe nyumba inakuwa na sehemu za uwazi wa wastani wa kupitishia hewa. Pia anasema lazima iwe na mlango na kufuli ambao utakuwezesha kumpitishia wakati wa kumfungulia kwa ajili ya ulinzi na pia wakati anarudi ndani.

Kadhalika, anasema lazima kuwekwe na sehemu nzuri ndani ya nyumba hiyo ya mbwa ambayo itatumika kumtengea chakula ambayo itamwezesha kula kwa uhuru.

Chacha anasema pia lazima uhakikishe kwamba unamwekea kifaa maalum ndani ya nyumba yake ambacho kitatumika kuhifadhia maji yake ya kunywa.

Anasema nyumba ya mbwa inahitaji kufanyiwa usafi kama ilivyo nyumba ya binadamu, na kuna umuhimu wa kuhakikisha usafi huo unafanywa mara kwa mara ili kumuepusha na maradhi.

Kwa mujibu wa Chacha, nyumba ya mbwa hujengwa ndani ya uzio wa nyumba ya kuishi binadamu, ni lazima suala la eneo la kujengewa nyumba hiyo ya mbwa lizingatiwe.

"Tunajua kwamba nyumba za mbwa kwa kawaida huwa siyo kubwa, na wengi wetu hupendelea kujenga au kuezeka na vitu vya ajabu ajabu ambavyo wakati mwingine inaweza kusababisha kuharibu muonekano mzuri na madhari ya nyumba, pia kama unaona itaharibu ni vema ujenge ambayo unaweza kuihamisha.


"Unaweza kuingia katika baadhi ya makazi ya watu, wanakuwa na nyumba nzuri, lakini unakuta hapo katikati ya nyumba wamejengea kibanda cha mbwa kibaya hadi kimeharibu kabisa fasheni ya nyumba. Kwa hiyo siyo vibaya kuchagua eneo zuri la kuweka vibanda hivyo," anasema.

Anasema nyumba ya mbwa pia inaweza kupakwa rangi kama zinazotumika kupaka katika nyumba wanazoishi binadamu.

"Kama unathamini kazi kubwa ya ulinzi inayofanywa na mbwa wako nyumbani, lazima pia uthamini maisha yake na makazi yake. Ikiwezekana paka rangi ya nyumba yake, weka hata vyombo na chakula bora kwenye nyumba yake na hii itasaidia awe na afya bora,"anasisitiza Chacha.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
LOH!
WA MITAANI
NAOMBA USHAURI NIMEMFUMANIA MKE WANGU MARA TATU.
SUBIRI MPAKA ANGALAU MARA NANE NDIO UJE
MWENE-KITI WA MTAA
UKATILI
TUONDOKE TUSHAFUKUZWA KAZI AU BADO HUAMINI
SIAMINI KAMA NINAYEKUONA NDIO UMEIBA HESABU UMELEWEA
HAPA MTU ANILETEE MADHARAU NDIO ATANIJUA KAMA NIKIWA 'BWIII' STAMINA NDIO ZINAKUJA
AROO WEWE UMEFIKAJE HAPA HEBU JIEREZEE
NIRUDISHE ULIPONIKAMATIA NITAKUMBUKA
POSTI
HIYO PETROLI UNAYONUKIA NIKURUDISHE WAKAMALIZIE?
BEBI ZILE ZILIKUWA SWAGA TU, SIJAWAHI KUWA TENESKO
KAMA MUOGA UKISHUKA HAPO NENDA KWA MKEO
*KINYUNYIZO CHA LEO...
SIO MAISHA TU HATA SIKIO UNATOBOA....

# WHO kupeleka chanjo ya Mpox DRC

**NEWYORK,** MAREKANI

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limesema kuwa shehena ya kwanza ya chanjo ya virusi vya homa ya nyani (mpox ) inatarajiwa kuwasili nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo siku chache zijazo.

Hayo yalielezwa na mkuu wa shirika hilo, Tedros Adhanom Ghebreyesus baada ya kurejea katika ziara yake ya nchini DRC.

Agosti 14, mwaka huu, WHO ilitangaza ugonjwa wa Mpox kuwa hali ya dharura ya kimataifa kutokana na kusambaa kwa kasi na kuongezeka kwa visa vya maambukizi vya aina mpya ya virusi hivyo inayofahamika kama Clade 1b nchini DRC na nchi jirani.

Kwa mujibu wa WHO, karibu visa 15,000 vya mpox vimegundulika ndani ya DRC kwa mwaka huu, huku vifo vikifikia 500.

Serikali ya Ujerumani ilisema itapeleka nchini humo maabara ya kuhamishika ili kusaidia kuwagundua wagonjwa wa homa ya Mpox na kudhibiti kuenea kwa maambukizi.

Wizara ya Ushirikiano wa Kimaendeleo wa nchi hiyo ilisema ina mipango ya kutoa mafunzo kwa wataalamu zaidi ili waweze kutambua dalili na kuufahamisha umma kuhusu hatua za kuzuia ugonjwa huo.

Kwa upande mwingine, Serikali ya Uingereza iliahidi kutoa pauni milioni 3.1 kwa ajili ya kusaidia kupambana na mlipuko wa homa ya Mpox.

**DW**

# Zelensky amtimua kamanda kikosi cha anga

**KYIV**, UKRAINE

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amemwondoa madarakani kamanda wa kikosi cha anga siku chache baada ya ndege mpya ya kivita aina ya F-16 kuanguka.

Ndege hiyo ni miongoni mwa ndege za kivita zenye gharama kubwa ambazo nchi hiyo imepewa na mataifa ya magharibi kama msaada katika vita vinavyoendelea na Russia.

Hata hivyo, Rais Zelensky hakutaja sababu ya kumfukuza kazi Luteni Jenerali Mykola Oleshchuk, lakini alisema ana jukumu la kuwatunza wapiganaji wote.

Ndege hiyo aina ya F-16 iliyotengenezwa Marekani ni moja ya ndege kadhaa zilizotolewa mwezi huu na washirika wa Magharibi kwa Ukraine.

Ingawa kuanguka kwa ndege hiyo kulitokea wakati wa msururu wa makombora yaliyorushwa na Russia, Ukraine ilisema chanzo cha ajali hiyo haikuwa matokeo ya moja kwa moja ya shambulio la adui.

Luteni Jenerali Oleshchuk alikuwa na wakati mgumu baada ya baadhi ya wanasiasa kuhoji nani alaumiwe kutokana na hasara hiyo.

Wakati huo huo, mtoto mwenye umri wa miaka 14 ameuawa baada ya shambulio la bomu lililofanywa na vikosi vya Russia katika mji wa kaskazini-mashariki wa Kharkiv.

Maofisa wa eneo hilo walisema watu wengine sita waliuawa na 59 kujeruhiwa wakati jengo la makazi la ghorofa 12 liliposhambuliwa katika mji ulioko karibu na mpaka wa Russia.Picha zilionesha miali ya moto na moshi mzito mweusi ukitoka sehemu ya juu ya jengo hilo huku wazima moto wakiwabeba watu na kuwapeleka maeneo salama.

Rais Volodymyr Zelensky, alitoa wito mpya kwa washirika wa kimataifa kuiruhusu kulenga maeneo ndani ya Russia ili kuzuia mashambulizi kama hayo.

Ofisi yake ilisema kuwa vikosi vya Russia vilirusha zaidi ya ndege 400 zisizo na rubani na makombora dhidi ya Ukraine katika muda wa wiki moja iliyopita.

**BBC**

# Ujerumani yaondoa wanajeshi Niger

**NIAMEY,** NIGER

KIKOSI cha mwisho cha wanajeshi wa Ujerumani kimeondoka Niger, hatua inayohitimisha operesheni zake katika ukanda wa Sahel.

Maofisa waandamizi wa jeshi la Ujerumani nchini Niger, walisema wanajeshi 60 walioondoka Ijumaa pamoja na tani 146 za vifaa vilivyosafirishwa na ndege tano za mizigo.

Mnamo Mei, mwaka huu Niger ilikubali kuruhusu wanajeshi wa Ujerumani kuendelea kuendesha shughuli zao katika kambi yao ya wanaanga iliyoko mjini Niamey.

Hata hivyo, mazungumzo yaligonga mwamba kati ya pande zote mbili baada ya Niger kushindwa kuhakikisha kwamba majeshi ya Ujerumani yaliyoko nchini humo yangenufaika na kinga dhidi ya kufunguliwa mashtaka.

"Kujiondoa kwao hakuashirii mwisho wa ushirikiano wa kijeshi kati ya Niger na Ujerumani," maofisa kutoka nchi zote mbili walisema katika taarifa ya pamoja iliyosomwa.

Kauli hiyo ni tofauti na ile ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Annalena Baerbock, ambaye alisema mwezi Julai kuwa hawawezi tena kushirikiana na Niger kwa sababu ya kukosekana kwa uaminifu.

Ujerumani ilianza operesheni katika kambi yake ya wanajeshi wa anga 2016, na ilikuwa na wanajeshi 3,200.

Taifa hilo lilichangia katika vita dhidi ya waasi katika nchi jirani ya Mali, kama sehemu ya ujumbe wa Umoja wa Mataifa wa kulinda amani ambao ulilazimika kukatisha shughuli zake mwaka jana.

**DW**



Wahamiaji wakiwa wametelekezwa eneo la jangwani na kukabiliwa na hatari ya kufa kwa kukosa chakula katika mpaka wa Tunisia na Algeria hivi karibuni. **PICHA: ALLIANCE**

# Wahamiaji waliotelekezwa jangwani waokolewa Tunisia

**TUNIS,** TUNISIA

SHIRIKA la kutetea haki za binadamu nchini Tunisia la FTDES limewaokoa wahamiaji 28 waliokuwa wametelekezwa jangwani katika mpaka wa Tunisia na Algeria.

Kulingana na shirika hilo, wahamiaji hao waliokolewa wakiwa katika hali mbaya kutokana na kukosa maji na chakula ni wanawake saba, watatu kati yao wakiwa ni wajawazito pamoja na watoto wawili.

Msemaji wa shirika hilo Romdhane Ben Amor , alisema walifanikiwa kuwaokoa kwa msaada wa mamlaka za ndani na walinzi wa taifa hilo ambao waliwapeleka katika kituo cha polisi. Ben Amor alisisitiza kwamba ni wazi kuwa wahamiaji wengine wako mafichoni na wanahofia kukamatwa na polisi. Wahamiaji hao watahamishiwa katika makazi yaliyo chini ya Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM).

Awali, shirika hilo liliripoti kuwa waomba hifadhi 42 nchini humo walifukuzwa kutoka mji wa Pwani wa Sfax na kupelekwa katika eneo hilo la mpaka.

Tunisia imekuwa kituo kikubwa cha wahamiaji wasio na vibali wanaojaribu kwenda Ulaya kupitia Bahari ya Mediterania.

**DW**

## MAKALA

# TUMEPATWA NA NINI?



Na Magabilo Masambu

**Wakati huo nikiwa naishi Mtibwa mkoani Morogoro, nyakati za jioni, nikiwa matembezini nilihisi kuna mtu ananifuata kwa nyuma.**

UKISIKILIZA na kutazama kwenye vyombo vya habari au kusoma magazetini kuhusu taarifa za matukio nchini mwetu kwa vyovyote lazima ujiulize tumepatwa na nini? Nini kimetokea cha tofauti kusababisha kila siku kusikia taarifa za kuogofya?

Je, kama taifa tunapaswa kunyamaza na kujifanya kwamba hatuoni kinachoendelea au tunapaswa kuzungumza na ikiwezekana tufahamu chanzo pamoja na utatuzi wake?

Kuna taarifa za watu kupotea au kuuawa na kidogo kidogo zinaanza kuonekana kama taarifa za kawaida masikioni mwetu. Ziko zinazohusisha imani za kishirikina, wivu wa kimapenzi, lakini zingine ni tuhuma juu ya baadhi ya vyombo vya usalama si jambo jema hata kidogo.

Zamani nikiwa kijijini, kuna wakati kulitokea taarifa fulani kwamba kuna mtu anatafuta kuua mtu fulani ili akafanyiwe tambiko. Taarifa hizi zilisikika mara kwa mara hasa nyakati za mavuno lakini baadaye nilikuja kufahamu kuwa kuna kitu kinaitwa misimu. Haya ni maneno au uvumi unaosambaa kwa haraka katika kipindi fulani na baadaye kupotea lakini ilipotokea hivyo pale kijijini tulikuwa tunaishi kwa hofu kubwa na wakati wa kuchunga mifugo tulilazimika kuchungia karibu na maeneo ya nyumbani na kurudi mapema nyumbani na ilipotokea ukakutana na mtu porini humfahamu ilikuwa lazima kutimua mbio kwa hofu iliyotanda.

Kwa sasa ni wazi kuwa Watanzania tumeanza kuishi kwa kuogopana. Zamani ilikuwa rahisi kumwambia mtu akuoneshe njia ikiwa umepotea lakini sasa mtu akijua umepotea njia anaweza kukuelekeza ili upotee zaidi. Nakumbuka kisa cha mtu mmoja niliyemsaidia mwaka 2002 na baadaye akaja kuwa msaada kwangu. Wakati huo nikiwa naishi Mtibwa mkoani Morogoro, nyakati za jioni, nikiwa matembezini nilihisi kuna mtu ananifuata kwa nyuma. Nilipungudua kwamba ananifuata nikapunguza mwendo ili apite lakini akasimama na kuomba kuzungumza na mimi.

Akaniambia ametoka Dodoma na amekuja kumtafuta ndugu yake anayefanya kazi katika kiwanda cha sukari Mtibwa, lakini hakuwa na mawasiliano yake na kwa sababu alifika jioni na hakuwa na mahala pa kulala. Kwa hiyo aliniomba kama inawezekana nimtafutie mahali pa kulala ili kukicha akamtafute huyo ndugu yake.

Nilifanya kama alivyoomba kwa sababu nyumbani hapakuwa na nafasi ya kutosha, nikampeleka nyumba ya kulala wageni Madizini na kwa sababu ilikuwa siku ya mwaka mpya vyumba vyote vilichukuliwa, nikamwomba mhudumu kwamba nalipa pesa lakini alale kwenye makochi sehemu ya mapokezi, akakubali. Nikamwacha hapo na kumwahidi kumwona kesho yake saa 4:00 asubuhi ili kumsaidia kumtafuta huyo ndugu yake na kwa sababu hakuwa na pesa yoyote.

Asubuhi nilimfuata na kumleta nyumbani ili kupata kifungua kinywa. Baada ya hapo tulianza kumtafuta ndugu yake na kwa bahati nzuri tukampata na safari yangu ikaishia hapo.

Baada ya takribani miaka sita, nilichaguliwa kwenda kusoma katika Shule ya Ufundi Ifunda Iringa. Siku moja tukiwa tumekwenda Iringa mjini kutembea, nikiwa maeneo ya stendi, nashtukia naitwa kwa jina langu. Nilipogeuka, aliyeniita sikumgundua kwa haraka maana sasa amebadilika na maisha yamekubali. Aliniuliza unanikumbuka? Nikasema hapana.

Jibu alilonipa ni kwamba wewe ulinihifadhi siku nimekuja Mtibwa kumtafuta ndugu yangu. Aliposema hivyo akalia. Kwa kweli hata mimi nilitokwa na mchozi, hivyo akaniomba nifike kwake na kuanzia hapo ndiye akawa mwenyeji wangu nilipokuwa nafunga shule sikuwa narudi Morogoro, mpaka leo mimi na jamaa huyo tumekuwa ndugu kama wa kuzaliwa baba na mama mmoja.

Nachotaka kusema ni nini? Upendo wetu kama Watanzania unaelekea kupotea kabisa. Zamani ilipopigwa mbiu au kelele juu ya tatizo fulani lililompata mwenzetu, tulitoka wote. Leo upendo huo umekwenda wapi? Zamani haikuwa rahisi mwenzetu aonewe na sisi tuko pale tumtazame lakini leo mtu anaweza kuchukuliwa na watu wasiojulikana mchana kweupe anakwenda kama kondoo na hatuwaulizi wanampeleka wapi. Umoja wetu nani ameuvuruga? Tumesikia ya Singida unajiuliza hivi mpaka mtu anafikisha watu 10 kuwaua na kuwazika hakuna hata mmoja alijua mapema na kama yupo hatua gani alichukua?

Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, aliacha taifa lenye umoja, upendo na Amani. Juhudi hizo zimeendelea kujengwa lakini kama alivyosema kwamba, sasa zipo nyufa mara hii si za ukabila wala udini bali nyufa za kuvunja umoja, upendo na amani na zisipodhibitiwa zitabomoa misingi tuliyo nayo kama taifa. Iwe ni kwa sababu ya siasa, ushirikina au mapenzi kama taifa hatupaswi kuona ni jambo la kawaida kwa sababu kila siku linakua na litakapokomaa kabisa watu watachinjana hadharani, juhudi za kukemea maovu haya lazima zifanywe na yeyote.

Vyombo vya ulizi vinapaswa kulinda umoja, upendo na amani waliyo nayo wananchi. Mambo hayo yakipotea kwa wananchi wenyewe itakuwa kazi ngumu sana kwa vyombo vya ulinzi kuhakikisha mambo hayo yanakuwapo. Tupendane tuthaminiane kama kuna shida tunapaswa kuzungumza lakini Jeshi la Polisi lina wajibu wa kisheria kulinda watu na mali zao kama watu wanapotea na halijui basi kuna kila sababu ya kuchukua wajibu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Arusha-Tanzania**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Kwaheri, penzi limeisha yabidi sasa tusahauliane*



Na Adam Fungamwango

**"Dada aaa, mpenzi kwaheri japo katika majonzi yangu, nasema nikitumaini ee kabisa kuwa utayajutia maisha, yetu pamoja."**

MWANAMUZIKI Dk. Remmy Ongalla katika wimbo wake mmoja alisema mapenzi yana matabaka matatu. Akasema mwanzo wa mapenzi utamu kama chungwa na katikati inakuwa uchachu kama limau au ndimu.

Akamalizia kusema mwisho wa mapenzi ni uchungu kama shubiri. Shubiri ni moja kati dawa chungu zaidi. Ni chungu kweli kweli.

Wengi hukwepa kutaja sehemu ya tatu ya mapenzi, pale wapendanao wanapochokana na kuanza kutafutiana visa vya kuachana.

Mwingine anaanza kuwa mbali na mwenzake, hapokei simu, au hata akipokea haongei maneno ya huba aliyokuwa akiongea hapo mwanzo. Hapo ujue tu kuwa penzi limefika tamati.

Lakini kwa nini penzi huwa linafika tamati kwa baadhi ya wapendanao au wanandoa? Hawakuendana? Kuna wapenzi miaka nenda rudi unaweza ukafikiri walianza kupendana jana. Kuna wanandoa ambao miaka ya ndoa inavyozidi kusonga mbele, ndoa inanawiri na kushamiri na kuwashangaza wengi.

Tunakuja kwa wale ambao baada ya muda penzi linachuja. Ndoa inavunjika, tatizo ni nini? Ni kwamba walipendana kwa mihemko. Ndiyo. Kuna wanaopendana kwa mihemko ya tamaa ya mali au kipenzi tu, lakini hawakupata muda wa kuchunguzana kama tabia zao zinaendana.

Wapenzi wanaodumu au ndoa zinatokana na wapendanao kuwa na tabia zinazofanana kwa asilimia 100 au walau 70 na kuendelea. Watu wanaokuwa na tabia zinazofanana huwa kila mmoja anapenda kukutana na mwenzake ili wazungumze kile ambacho huwa wanazungumza, ambacho kwa mwingine hawezi kukipata. Hii inakwenda mpaka kwa marafiki. Mtu unaweza kushangaa kwa nini fulani ni rafiki sana wa fulani. Ukichunguza utakuta tabia zao zinaendana, hata kama ni mbaya, lakini zinafanana.

Mwanzoni mwa miaka ya 1970, mwanamuziki Patrick Balisidya alitunga kibao alichokiita 'Yabidi Tusahauliane.'

Maudhui ya wimbo huu yanaakisi hiki ninachokisema. Mwanaume mmoja alimpenda msichana bila kuangalia kama wanaendana. Kila mmoja anamkubali mwenzake kwa ajili ya mihemko. Halikudumu. Kila mmoja akamchoka mwenzake. Wakaachana na penzi likafa kifo cha kawaida. Mashairi ya wimbo huu yanaanza hivi.

"Dada aaa, sikutegemea kusahauliana naye kamwe, kwa jinsi dada nilivyokupenda, lakini ninayakini kuwa yabidi tusahauliane."

Jamaa anakiri kuwa alimpenda sana msichana huyo, lakini kwa jinsi ilivyo sasa, inabidi tu wasahauliane, kila mmoja ashike lake.

"Dada aaa, mpenzi kwaheri japo katika majonzi yangu, nasema nikitumaini ee kabisa kuwa utayajutia maisha, yetu pamoja."

Mwanaume anamwambia mpenzi wake kuwa wanaachana japo kwa majonzi, lakini ipo siku mwanamke atayakumbuka maisha ambayo walikuwa wakiishi pamoja. Ni kweli yale maisha ya mwanzo wa mapenzi yanakuwa ya kubembelezana kama njiwa.

"Dada aaa, kweli utengano wetu ni kitu kichungu, lakini si kigeni katika maisha ya kila siku, tafsiri yako na yangu, zimegongana."

Jamaa anakiri kuwa kuachana ni kuchungu lakini si kitu kigeni katika maisha ya kila siku ya mapenzi, na wanaachana kwa sababu hawaelewani, tafsiri zao au lugha zinagongana. Huyu akisema hili, mwingine anafanya vile.

"Neno hili upendo na imani zetu zimekuwa si sawa eee dada, neno hili upendo limekuwa ni sumu, limetulitea kufarakana."

Ni kweli, walipendana kimihemko, sasa pendo limekuwa sumu, limewasababishia kufarakana.

"Hivi ndivyo inavyokuwa mara nyingi dada kwa hiyo kuwa na pendo kama sisi dada aaa. Eee nadhani tulikosea kufanya pupa iii kweli dada. Eee ingefaa tujichunguze kwanza nafsi zetu sana dada aaa. Eee na tuichunguze sana ukweli wa misimamo yetu ooo.

Katika jambo hili hatukufanya hivyo ole wetu ole wetu ooo dada. Haya ndiyo makosa yafanywayo katika kisingizio cha upendo dada."

Jamaa anarudia mle mle, hawakuchunguzana kwanza, tabia, misimamo kabla ya kuingia kikamilifu kwenye penzi, ana anakiri kuwa walifanya pupa, huku akisema haya ndiyo makosa yanayofanywa na watu wengi kwa kisingizio cha upendo. Mwisho kabisa anamuaga mpenzi wake huyo ambao kuanzia wakati huo anakuwa 'ex' wake 'bai bai.'

Hapa tunajifunza kitu kimoja. Unapofanya uchaguzi, fanya ulio sahihi. Usichangue mpenzi kwa sababu ya shepu, macho, weupe, weusi, au kitu chochote ambacho baadaye kwa mpenzi wako kinaweza kutoweka, au ukakizoea na kuwa cha kawaida. Kumbuka unayemchagua ni mpenzi ambaye utakuwa naye mara kwa mara, hivyo ni lazima hata tabia na mienendo inabidi ifanane ili kila mmoja amfurahie mwenzake badala ya 'kuboa.'

Hata watoto wa kike wanatakiwa kukubali wanaume si kwa sababu ya pesa, umaarufu au kitu kingine kinachofanana na hicho.

Wanaume wanaotakiwa kuwa nao ni wale ambao wanaweza kuwa huru na kujisikia amani na furaha wanapokuwa pamoja. Na hii haiwezi kuja kama tabia zetu haziendani. Kila mmoja atamchoka mwenzake baada ya siku chache tu.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Aka Simtaki-9

BAADA ya kumaliza masomo yake ya kidato nne na kushindwa kuendelea na masomo kutokana na hali duni ya wazazi wake, Shani alitakiwa kuolewa. Akakubali, lakini ni kwa yule ambaye anampenda. Haikuwa hivyo, kwani baba yake mzee Chilambo alimlazimisha aolewe na mwanamume mwenye uwezo, mali na fedha ili asiende kuteseka. Tatizo likaanzia hapo, mwenye pesa hakupendwa na Shani, asiye na uwezo alikuwa kwenye moyo wake. Baba anamtaka mwenye uwezo. Jambo hili linazua mgogoro mkubwa kwenye familia tatu, za binti na wachumba wawili. Nini kitatokea. Usikose kila nakala ya gazeti hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

AKILI yake ilimtuma kutafuta watu wengine kwa kutumia pesa za wazazi wake, kufanya uchunguzi wa kina ni kwa nini barua imekubaliwa, lakini badala ya taratibu na maandalizi ya harusi kufanyika, badala yake wanasema kuwa majadiliano? Na ni kweli kwamba binti huyo ameweka ngumu? Kuna ukweli gani kuwa kuna mwanaume kwenye kijiji hicho ambaye ni mpenzi wake? Je na yeye pia alipeleka barua? Alijibiwa vipi? Je Shani ameweka ngumu kuolewa na yeye kwa sababu ya kijana huyo au kuna kitu kingine zaidi? Je ni nani kijana huyo? Jina lake, uwezo wake na familia anayotoka. Majibu yatakayopatikana ndiyo ataamua yeye afanye nini ili kufanya chochote kitakachowezekana Shani aingine mikononi mwake.

"Haya tunaona kama nitamuoa au simuoi." Akasema Fotu kwa ajili ya kutaka kuumaliza mjadala, kwani tayari kichwani mwake alishatengeneza mpango mkakati huo kabambe.

"Sasa Nyendo ndiyo umemuacha kabisa, maana nayeye anataka kuolewa yule, akipata mchumba je?"

"Akipata aolewe, mimi akili yangu yote ipo kwa yule msichana wa Lalangulu, siyo huyu wa hapa Mtapenda."

"Mimi nina wazo moja!" "Lipi?" "Usimuache, ili dili likibuma kabisa umarudia Nyendo, nadhani ukimuomba tu msamaha anaweza kukuelewa."

*******************************

"Wewe kijana nasikia unatoka kijiji cha Mtapenda!" "Ndiyo kwani vipi?" "Ukifika huko, nenda kamwambie kijana mmoja anaitwa Fotu asijione mjanja sana kwa kumtorosha mpenzi wangu. "Mpenzi wako?" "Ndiyo, huyo Fotu wenu baada ya kuona hatakiwi, kashawishi kwa vipesa vyake mpaka kabadili mawazo."

Ilikuwa ni sauti ya Shukuru ikimwambia kijana mmoja ambaye alikuwa amepaki bodaboda yake akinunua bidhaa dukani. Kuna mtu alimtonya Shukuru kuwa kijana yule anaishi kijiji jirani cha Mtapenda. Taarifa ambazo hazikufanyiwa uchunguzi na kumfikia ni kwamba mpenzi wake Shani ametoroshwa na Fotu.

Mara nyingi taarifa za tetesi, huwa zinatiwa chumvi wakati mwingine hadi kumfikia mlengwa zinakuwa zimepindishwa kisawasawa.




**"Si hivyo Shani, kama kuna watu ambao wameshaleta barua kwenu na wazazi wako wamei-kubali na ya kwangu wameipiga chini, wewe si wa kwangu tena." Akasema Shukuru kwa uchungu.**

Shani ametoroka nyumbani kwao kwenda kijiji cha Ilembo, baada ya baba yake mzee Chilambo kulazimishwa kuolewa na mwanaume asiyempenda. Lakini alichokipata Shukuru ni kwamba Shani ametoroshwa na Fotu, kijana ambaye wanamgombea msichana huyo. "Sasa wewe umeshindwa vipi kwenda kumwambia?" Akaulizwa swali. "Ndiyo nakutuma hivyo, mimi nikifika huko itakuwa vita, sijali ana uwezo au mtoto wa tajiri." "Ndugu yangu, wewe unamuogopa, hujiamini, kama kweli mpenzi wako wamechukuliwa, si ungemfuata kwani Mtapenda mbali? Au nikupe lifti kwenye bodaboda yangu nilipeleke hadi nyumbani kwake?" Kijana yule alizidi kumbana na kumpa wakati mgumu Shukuru. "Nitakuja kwa wakati wangu, wewe kampe taarifa." Akajibu Shukuru. Kijana mwenye bodaboda mkazi wa kijiji cha Mtapenda alikuewa ameshaiwasha na taratibu akaanza kuondoka, lakini hakumuacha Shukuru hivi hivi, akamuacha na neno. "Ushafeli ndugu yangu."

*******************************

Shani alikaa kwa kina Salum na Dora, mtu na dada yake kwa muda wa wiki moja. Tayari alikuwa ameshawazoea wote wawili, hivyo jioni wanapotoka shambani, wanamkuta amepika chakula, wanakuka na kutandika mkeka nje ya nyumba na kupiga stori.

Shani alikuwa ameshawaambia wenyeji wake ni kitu gani kimemsababisha kuwa pale siku zile walipomkuta amelala.

Aliwaambia kuwa alikuwa akielekea kusikojulikana na ulipofika usiku aliamua kulala pale ili asubuhi akiamka aendelee na safari asiyoijua. Hakujali hata kama angeliwa na mnyama yoyote. Hakuona tena kama anastahili kuishi. Ndugu hao walimpa pole, wakampa kila aina ya ipendo kiasi cha muda mfupi tu kusahau kila kitu kilichomtokea.

Angeendelea kuishi huko kama si taarifa za kiitelejensia zilizopelekwa kwa wazazi wake na serikali ya kijiji kuwa yupo huko. Walitumwa watu wa ulinzi shirikishi ambao walitumwa kwenda kijiji cha Ilembo na kumkuta huko.

Walichofanya ni kumchukua tu kwa sababu hata serikali ya kijiji hicho ilikuwa na taarifa kuwepo kwa mgeni huyo na sababu, hivyo hakuona ulazima wa kumrudisha, badala yake wakaona akae hapo hadi ndugu na jamaa wanapokuja kumchukua wenyewe.

Shani aliwashukuru Salum na Dora, akiwaahidi kuwa kuna siku atarejea kwani ameshakuwa kama ndugu yao, nao wakamkaribisha muda wowote wa saa yoyote anaweza kwenda.

"Haya mwanangu, kilichokufanya wewe utoroke nyumbani ni kitu gani? Mimi mama yako, sili, siogi, sinywi, silali kwa ajili yako binti yangu." Shani hakujibu kitu akabaki anamuangalia mama yake.

"Shani, nakuuliza mwanangu, ni ktu gani kimesababisha mpaka hata mimi mama yako unanitoroka, nalia mimi usiku kucha, kumbe umeenda kujificha kwenye majumba ya watu, sijapenda." Yalikuwa ni maneno ya Bi Hanifa, mara baada ya binti yake kurudishwa na vijana wa ulinzi shirikishi wa kijiji hicho cha Lalanguru kutoka kijiji cha jirani cha Ilembo. Bado Shani alikuwa kimya, akimwangalia mama yake kwa huzuni, lakini hakunyanyua mdomo wake kuongea lolote.

****************************

Shukuru aliposikia kuwa mpenzi wake amerejea na kumbe hakutoroshwa na Fotu, bali alitoroka mwenyewe kwa kulazimishwa kuolewa.

Hili lilimpa nguvu kutaka kwenda nyumbani kwao. Aliona kama alitoroka na sasa amepatikana inawezekana wazazi wake hasa baba yake akaamua kusalimua amri. Hakuwa hivyo. Akaishia kutimuliwa na mzee Chilambo.


Kurejea kwa Shani kulimfanya mzee Chilambo na ndugu zake kuendelea na matayarisho ya harusi. Upande wa mwana harusi ukapelekewa taarifa kuwa ujiandae. Ni baada ya mahari kubwa kulipwa. Ilivunja rekodi ya vijiji vyote vya Ugalla.

Kama utamaduni ya harusi nyingi kwa sasa, hasa za watu wanaojiweza. Mialiko ikaanza na kadi zikaanza kutembezwa katika kijiji cha Mtapenda ambacho anatoka bwana harusi na kile cha Lalangulu cha bi harusi. Pia vijiji jirani navyo ndugu na marafiki walialikwa kwenye harusi hiyo, kikiwemo cha Ilembo ambacho anatoka Salum na dada yake Dora. Taarifa hizo pia zikamfikia Shukuru. Ilikuwa ni taarifa mbaya kuwahi kutokea maishani mwake. Kuambua tarehe na siku ambayo mpenzi wake aliyetarajia kumuoa yeye anaolewa na mwanaume mwingine.

Hakuamini anachokisikia. Kila kitu kwake aliona kama ndoto. Yote aliyofanyika aliona kama yanaweza kufeli kwa sababu aliami Shani anampenda kwa dhati na asingeweza kamwe kuolewa na mwingine hata kama baba yake atalazimisha. Binafsi aliona maisha yake yaliyobaki bila ya kuwa na Shani hayatokuwa na thamani tena.

Afadhali kama angekuwa amefariki angeweza kushukuru Mungu, lakini kwa mtu anayempenda, yupo hai, akimuona yupo na mtu mwingine, akimpikia, kumfulia, kumtunza na kumfanyia kila kitu kama mumewe yeye akishuhudia, hakutaka kukutana na kitu kama hicho. Akawa anawaza ni kitu gani anaweza kufanya ili kuepuka kushuhudia kitu kama hicho. "Niondoke hapa kijiji?" Akawaza.

**Itaendelea Jumapili**



# UMEMWONA MASHA LOVE?

MWIGIZAJI Masha Love, amesema tayari ndugu wa mpenzi wake Moses Iyobo wanamtambua na wakati wowote watafunga ndoa kama taratibu zote zitakamilika.

Masha Love amesema kwamba hakuna tatizo na kile anachokifanya katika mitandao ya kijamii, kwani akiwa nyumbani anakuwa tofauti na hivyo hana matatizo na wakwe zake.

"Taarifa nzuri ni kwamba nimechumbiwa, baba na mama mkwe wanajua kama mimi ni mkamwana wao, hawawezi kuona matatizo kutokana na kazi yangu nikiwa kwenye mitandao ya kijamii," amesema Masha.

# HUYU HAPA STANS

HATIMAYE mwanamuziki wa Bongo Fleva, Marioo ametuliza joto la mashabiki wake baada ya kujulikana Stans, kuwa ndiye msanii wake wa kwanza katika lebo yake ya Bad Nation.

Katika siku kadhaa, Marioo aliwafanya mashabiki wa muziki kuwa roho juu kujua nani atamtambulisha kama msanii wake na kusababisha mitandao ya kijamii kuwa ya moto.

Marioo anakuwa msanii wa tano nchini kumiliki lebo, wengine ni Diamond Platnumz, Harmonize, Rayvanny, Nandy na Alikiba.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GUEHI ATAKIWA LIVERPOOL
LIVERPOOL inaweza kumnunua beki wa kati wa Crystal Palace na England, Marc Guehi, mwenye umri wa miaka 24, msimu ujao wa joto, wakati atakuwa amebakisha mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake. Guehi alikuwa akilengwa na Newcastle United katika dirisha la usajili msimu huu. ***(Mirror)***

### UNITED YAIKATALIA REAL BETIS
KLABU ya Manchester United ilikataa ombi la Real Betis ili kumsajili kwa mkopo winga wa Brazil, Antony, mwenye umri wa miaka 24, na kiungo wa kati wa Denmark, Christian Eriksen (32), katika siku ya mwisho ya dirisha la usajili. ***(Mail)***

### OSIMHEN SASA KIMEUMANA
MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 25, hatajumuishwa katika kikosi cha Napoli baada ya kushindwa kupata uhamisho wa kwenda Chelsea. ***(Gianluca di Marzio)***

### DILI LA WASHINGTON LAKWAMA
MAZUNGUMZO ya kumnunua mshambuliaji wa Chelsea, Deivid Washington, kwa dau la pauni milioni 16.8 kwenda Strasbourg yaligonga mwamba baada ya kuhofia uhamisho huo ungechunguzwa kwa sababu klabu zote mbili zinamilikiwa na BlueCo. ***(L'Equipe)***

### NEWCASTLE YAGHAIRISHA
KLABU ya Newcastle United inaelekea kusitisha juhudi za kumsajili mlinzi wa England, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 24, baada kuchoshwa na mazungumzo ya muda mrefu na Crystal Palace. ***(Sky Sports)***

### LIVERPOOL YAIGOMEA FOREST
LIVERPOOL imekataa ofa ya fedha taslimu pamoja na mchezaji kutoka Nottingham Forest kwa ajili ya mlinda mlango wao wa Jamhuri ya Ireland, Caoimhin Kelleher, mwenye umri wa miaka 25. ***(Athletic)***

### ÉDOUARD ATAJWA IPSWICH
KLABU ya Ipswich inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Ufaransa na Crystal Palace, Odsonne Edouard, mwenye umri wa miaka 26 baada ya usajili wa mkopo wa mshambuliaji wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Albania, Armando Broja (22), kugonga mwamba. ***(Standard)***

### ALMIRON MAMBO MAGUMU
KLABU ya Fulham haitamsajili kiungo wa Newcastle United mwenye umri wa miaka 30 ambaye ni raia wa Paraguay, Miguel Almiron. (Mail)

### ZOUMA SAFARI IMEIVA
MLINZI wa West Ham Mfaransa Kurt Zouma, mwenye umri wa miaka 29, amekamilisha uchunguzi wa matibabu na anakaribia kukamilisha uhamisho wa awali wa mkopo kujiunga na Al-Orouba ya Saudi Pro League. ***(Sky Sports)***

### CHELSEA YAMTAKA ARAUJO
CHELSEA imemuuliza beki wa Benfica ambaye ni raia wa Ureno, Tomas Araujo, mwenye umri wa miaka 22. ***(Mirror)***

### NAPOLI YAMKOSA GILMOUR
KIUNGO wa Scotland, Billy Gilmour, mwenye umri wa miaka 23, hataweza kuhamia Napoli msimu huu baada ya kiungo mpya wa Brighton, Matt O'Riley, kuthibitishwa amepata jeraha baya kwenye mechi yake ya kwanza. ***(Telegraph)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DI MARÍA AFUNGUKA KUHUSU VAN GAAL

Mshambuliaji huyo asema alikuwa ni kocha mbaya zaidi kwake...

**BUENOS, Argentina**

SI mara nyingi wachezaji huwa na tabia ya kuwataja makocha wao wabaya zaidi, lakini Ángel Di María haonekani kuwa na tatizo hilo.

Akizungumza na ESPN Argentina, kiungo huyo wa kati wa Benfica na Argentina mwenye umri wa miaka 36 alichagua msimu wake mmoja katika klabu ya Manchester United chini ya Louis van Gaal, akitaja jina la kocha huyo wa Uholanzi kuwa mbaya zaidi alipoulizwa kubainisha makocha watatu bora katika maisha yake ya soka.

"Mbaya zaidi ni Van Gaal, naweza kuwa na uhakika wa hilo. Iwapo utakuwa na shaka yoyote, nitakuthibitishia hilo kwa sasa," alisema Di María akiiambia ESPN.

[redacted]

kumzungumzia vibaya Van Gaal.

Mnamo 2021, Di María alimwelezea kwa maneno sawa na hayo, kwa Van Gaal kabla ya pambano kati ya Argentina na Uholanzi kwenye fainali za Kombe la Dunia la 2022.

"Ángel Di Maria ni mchezaji mzuri wa soka," alisema Van Gaal wakati wake kama kocha wa timu ya taifa.

"Wakati alipokuwa akiichezea Manchester United, alikuwa na masuala mengi ya kibinafsi."

Di María aliendelea kufafanua Lionel Scaloni, ambaye alishinda naye Kombe la Dunia la 2022 akiwa na Argentina, kama "mmoja wa bora," pamoja na kocha mwingine wa timu yake ya taifa, Alejandro Sabella, ambaye "alikuwa na mchan-

[redacted]

nafasi maalum kwa hayati Diego Maradona, ambaye pia alimfundisha akiwa na Argentina.

"Sitamchukulia kama kocha kwa sababu kwangu alikuwa rafiki wa karibu zaidi, mtu ambaye alipita ili kuzungumza," alisema Di María.

"Hakuonekana kama kocha lakini zaidi kama rafiki, kaka, baba. Baba kuliko kitu chochote. Alinivumilia wakati hakuna mtu mwingine aliyefanya hivyo, alinisaidia kusonga mbele. Kadiri nilivyopokea ukosoaji zaidi, ndivyo alivyozidi kuniunga mkono.

"Alikuwa kila kitu kwangu. Diego ndiye bora zaidi kuwahi kuwa naye. Nimewahi kusema, Leo Messi ndiye bora zaidi wa wakati wote, lakini Diego ni Diego. Kwangu, kwa Argentina na kwa ulimwengu."

HABARI MICHEZO

# ARSENAL YAFANIKIWA KUMSAJILI STERLING

**LONDON, England**

ARSENAL imemsajili mshambuliaji wa Chelsea, Raheem Sterling, kwa mkopo kwa muda wote uliosalia wa msimu huu, klabu hizo zimethibitisha.

Sterling amebakiza miaka mitatu katika mkataba wake sasa na Chelsea lakini amekuwa akionekana ni ziada ya mahitaji ya Stamford Bridge.

Baada ya hapo awali kuhusishwa na Manchester United, Sterling alikamilisha uhamisho wake wa kwenda Arsenal kabla tu ya kufungwa kwa dirisha la usajili la majira ya kiangazi.

Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, aliitenga klabu hiyo kutoka kwa Sterling wiki iliyopita licha ya kuzungumza vyema kuhusu tabia yake baada ya wawili hao kufanya kazi pamoja kwa miaka mitatu huko Manchester City.

Hata hivyo, Arsenal wamekuwa tayari kusajili mchezaji wa kushambulia katika kipindi chote cha dirisha hili na wanajadili chaguo lao, huku pia wakihusishwa na kutaka kumnunua winga wa Bayern Munich, Kingsley Coman.

Uhamisho wa Sterling ulikuja baada ya Arsenal kumtoa winga mwenzake Reiss Nelson kwa mkopo kwa Fulham kwa msimu huu, huku Washikabunduki hao wakiamini kuwa Sterling angemboresha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24.

Pia Arsenal juzi ilitangaza kumsajili kipa wa Bournemouth, Neto, kwa mkataba wa mkopo wa msimu mzima.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 ametambuliwa na Arsenal kama mbadala wa kipa chaguo la kwanza, David Raya, huku kuwasili kwake kukimwezesha Aaron Ramsdale, kukamilisha uhamisho wake kwenda Southampton.

Kama ESPN ilivyoripoti Alhamisi, Ramsdale imekubali mkataba wenye thamani ya hadi pauni milioni 25 ikijumuisha nyongeza.



# Osimhen mambo magumu

**NAPLES, Italia**

MUSTAKABALI wa Victor Osimhen hauonekani baada ya Chelsea kushindwa kufikia makubaliano ya kumsajili mshambuliaji huyo wa Napoli kabla ya tarehe ya mwisho ya usajili wa England.

Vyanzo vimeiambia ESPN klabu ya Osimhen ya Juventus ilikubali ofa ya Euro milioni 80 kutoka kwa Al Ahli ya Saudi Pro League lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria alionyesha mashaka yake juu ya kuondoka soka la Ulaya.

Hilo liliwaacha Chelsea kushindwa kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25.

Lakini, vyanzo vimeiambia ESPN makubaliano hayakufikiwa kwa wakati.

Al Ahli pia walifuatilia mpango wa kumnunua mshambuliaji wa Brentford, Ivan Toney, na huku klabu hiyo ya Saudi Arabia ikishindwa kuwasajili washambuliaji wote wawili, sasa inaonekana Osimhen anakabiliwa na matarajio ya kusubiri klabu nyingine ya Mashariki ya Kati kufanya uhamisho wa kuchelewa -- dirisha la Ligi Kuu ya Saudia itafungwa kesho kujaribu kujenga upya uhusiano wake huko Napoli.

Osimhen atakuwa na vita kali huko Napoli baada ya kocha mkuu mpya Antonio Conte kufanikiwa kuisukuma klabu hiyo kumsajili Romelu Lukaku kutoka Chelsea kwa mkataba wa pauni milioni 30.



# Sancho atua Chelsea

**LONDON, England**

KLABU za Manchester United na Chelsea zimefikia makubaliano ya mkataba wa mkopo kwa Jadon Sancho, kwa mujibu wa ESPN.

Chelsea itamchukua Sancho kwa mkopo kwa msimu huu huku wakiwa na jukumu la kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu msimu ujao kwa ada ya karibu pauni milioni 25.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa England hajashiriki katika mechi ya ushindani kwa United kwa zaidi ya mwaka mmoja na aliachwa nje ya kikosi cha Erik ten Hag kwa mechi mbili za kwanza za Ligi Kuu England dhidi ya Fulham na Brighton.



Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 amebakiza miaka miwili kwenye mkataba wake Old Trafford.

Sancho alitumia kipindi cha pili cha msimu uliopita kwa mkopo katika klabu yake ya zamani ya Borussia Dortmund baada ya kuondolewa kwenye kikosi cha kwanza cha United kufuatia mzozo wa hadharani na Ten Hag.

Alijumuishwa tena msimu huu wa joto na akarejea mazoezini lakini licha ya kuwa na jukumu kuu katika ziara ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekaniameruhusiwa kuhamia kwa mahasimu wao wa Ligi Kuu Chelsea.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN United walikuwa na nia ya kufanya mazungumzo ya kumuuza Sancho kwa mkataba wa kudumu, lakini thamani ya takriban pauni milioni 40 imeonekana kuwa kikwazo kikubwa.

Chelsea walisonga mbele mbele ya Juventus katika mbio za kuwania saini yake baada ya mazungumzo na timu hiyo ya Italia kukwama siku ya Alhamisi. Maendeleo makubwa yalifanywa wakati wa majadiliano siku ya Jumatano lakini Juventus walishindwa kufikia makubaliano.

# HABARI MICHEZO

# TFF: TUMENOGEWA KUSHIRIKI FAINALI ZA MICHUANO AFCON

**Na Somoe Ng'itu**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), limesema timu yake ya Taifa Stars sasa imekuwa na uchu wa kushiriki kila fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), ambazo hufanyika kila baada ya miaka miwili, imeelezwa.

Taifa Stars inaendelea na mazoezi kwa ajili ya kuikaribisha Ethiopia katika mechi ya Kundi H ya kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika itakayochezwa Jumatano kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Baada ya mechi hiyo Stars itasafiri kuelekea Guinea kwa ajili ya mchezo mwingine wa kundi hilo utakaochezwa Septemba 10, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, aliliambia gazeti hili jana maandalizi yanaenda vizuri na anaamini Taifa Stars itapata tena tiketi ya kushiriki fainali hizo zitakazofanyika mwakani nchini Morocco. Ndimbo alisema kufanya vizuri kwa mchezo dhidi ya Ethiopia itatusaidia kupiga hatua kuelekea kufikia malengo ya kufuzu.

"Tumeanza kunogewa kwa kufanya vizuri kwa timu zetu za taifa, kwa wanawake, wanaume na michuano mbalimbali, ...kaka zao kina Adolph alicheza, tukaja kufuzu baada ya miaka 39, lakini tukacheza tena hizi zilizopita, tumepunguza muda," alisema Ndimbo.

Aliongeza kutopata tiketi ya kufuzu fainali za mwakani itakuwa ni 'deni' kwa timu yetu ambayo itakuwa mwenyeji kwenye fainali za mwaka 2027.

"Matokeo mazuri yatakuwa nguvu ya kufanya vizuri katika mechi ya pili ya ugenini, ingawa haikatazwi kupata ushindi ugenini, ukifanya vizuri kuanzia mwanzo unajipunguzia mlima, wachezaji wanajua hilo, benchi la ufundi wanatambua hilo, mdau namba moja kwa maana ya serikali anatambua hilo," Ndimbo alisema. Aliongeza kwa kuwaita mashabiki wa soka nchini kujitokeza kwa wingi uwanjani ili kufanikisha Stars inaanza vyema kampeni zake.

Naye Kiungo wa Stars, Feisal Salum 'Fei Toto' amesema wako tayari kwa ajili ya mechi hizo mbili na wanawaomba mashabiki wajitokeze kuwashangilia keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.



Wachezaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), wakifanya mazoezi ili kujiandaa na mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za AFCON dhidi ya Ethiopia itakayochezwa Jumatano kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# JKU, Chipukizi kibaruani Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MABINGWA wa Ligi Kuu Zanzibar, JKU wanatarajia kukutana na Chipukizi kutoka Pemba katika mechi ya Ngao ya Jamii itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan Complex.

Mechi hiyo ni maalumu kwa ajili ya kufungua rasmi pazia la msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar 2024/2025.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Chipukizi, Mzee Ali, alisema wamejiandaa vyema kucheza soka la ushindani ili kuhakikisha wanabeba ngao hiyo.

Ali alisema ingawa mchezo huo sio rahisi kama unavyozaniwa lakini mipango yao mikubwa ipo kuhakikisha wanaanza msimu mpya kwa 'kishindo' kwa kucheza kwa tahadhari.

"Tumejiandaa kuhakikisha hatufanyi makosa kuelekea mchezo huu muhimu wa ufunguzi wa ligi yaani Ngao ya Jamii, tunaamini kesho (leo) ni kupata ushindi na kuipata ngao ili kuwa na hamasa zaidi kuelekea msimu mpya," kocha huyo alisema.

Naye Kocha wa JKU, Salum Haji, alisema licha ya kuwa na majeruhi watatu wa kikosi cha kwanza lakini anakikosi kipana kitakachotetea ngao hiyo.

"Tunashuka uwanjani kwenda kuitetea ngao yetu ambayo mwaka jana tuliichukua na mwaka huu lengo kushinda kwa idadi kubwa ya magoli," alitamba.

# Maxi afurahia

INATOKA UK. 24

2022 kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, mechi hiyo iliisha kwa Yanga kupata ushindi wa mabao 2-1, Mayele akitangulia dakika ya 41, kabla ya Bakari Mwamnyeto kufunga la pili, Salum Kipemba akifunga bao la kufutia machozi kwa wenyeji.

Naye nahodha msaidizi, Dickson Job, ambaye msimu uliopita ndiye aliyefunga bao la kwanza kwa timu hiyo, ameeleza kufurahishwa kwake kuchangia bao la Nzengeli.

"Msimu uliopita mimi nilifunga bao la kwanza, msimu huu ilikuwa bado kidogo nianze na 'asisti', lakini nimechangia bao la kwanza. Ule mpira mimi ndiye niliyempa Maxi, sasa badala ya kwenda kufunga, yeye akampasia kwanza Stephane Aziz Ki, ndipo alipoharibu, halafu akamrudishia mwenyewe akaenda kufunga bao," alisema Job huku akicheka.

Msimu uliopita, Job alifunga bao la kufungulia msimu, Agosti 23 mwaka jana kwenye Uwanja wa Azam Complex, alipopachika bao dakika ya 16, Yanga ikicheza dhidi ya KMC, na kuibuka kidedea kwa mabao 5-0.

Mara ya mwisho Yanga kupoteza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara ilikuwa ni Septemba 20, 2014 ilipofungwa mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani, Morogoro dhidi wenyeji Mtibwa Sugar, mabao yaliyofungwa na Mussa Hassan 'Mgosi' na Ame Ally.

Simba ndio vinara wa ligi hiyo yenye timu 16, akiwa na pointi sita baada ya kushinda mechi zote mbili walizocheza sawa na Singida Fountain Gate huku Mashujaa FC ya Kigoma ikiwa kwenye nafasi ya tatu na pointi zake nne kibindoni wakati Yanga inafuatia ikiwa na pointi tatu.

Fountain Gate ya Singida iliyopanda daraja msimu huu inafuatia katika msimamo huo ikiwa na pointi tatu sawa na Tabora United ya mkoani Tabora.

Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kupisha kalenda ya kimataifa ambapo hapa nchini Taifa Stars itawakaribisha Ethiopia katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa Afrika itakayochezwa Jumatano kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

# Simba SC: Tutafurahi

INATOKA UK. 24

ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Tabora United na mchezo wake wa pili ikawafunga Fountain Gate magoli 4-0.

Nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara inashikiliwa na Singida Black Stars yenye pointi ikifuatiwa na Mashujaa FC ya Kigoma iliyojikusanyia pointi nne wakati Yanga inafuatia ikiwa na pointi tatu.

Fountain Gate ya Singida iliyopanda daraja msimu huu inafuatia katika msimamo huo ikiwa na pointi tatu sawa na Tabora United ya mkoani Tabora.

Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kupisha kalenda ya kimataifa ambapo hapa nchini Taifa Stars itawakaribisha Ethiopia katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa Afrika itakayochezwa Jumatano kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Michezo
Jumapili Septemba 1, 2024
Nipashe



Di María afunguka kuhusu Van Gaal UKURASA 21

## Simba SC: Tutafurahi

Na Somoe Ng'itu

HUKU wakiwa kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kupata ushindi wa mechi mbili walizocheza, uongozi wa Simba umesema wanakiamini kikosi walichonacho kitapambana na kuwafuta 'machozi'.

Simba jana ilikuwa inacheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Al Hilal kutoka Sudan ili kujiimarisha kuelekea mchezo wake wa Kombe la Shirikisho Afrika utakaochezwa ugenini Septemba 13, mwaka huu.

Wekundu wa Msimbazi itawafuata Al Ahly Tripoli ya Libya na baadaye itarejea nyumbani kwa ajili ya mchezo wa marudiano utakaochezwa Septemba 20, mwaka huu kwenye kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema timu yao imeshaanza kuwapa 'matunda' na wanaamini wachezaji wataendelea kuwapa furaha katika michezo inayokuja.

Ahmed alisema kila mchezaji anafahamu 'kiu' waliyonayo mashabiki na wanachama wa Simba hivyo jukumu lao ni kupambana na kusaka ushindi katika kila mechi watakayocheza.

"Tuna wachezaji wazuri na wakubwa, wanajua wanatakiwa kufanya nini na kwa wakati gani, pia tuna benchi la ufundi ambalo limetimia kwa ajili ya kuhakikisha malengo ya klabu yanafikiwa," alisema Ahmed.

Aliongeza wamejipanga kukutana na ushindani katika kila mechi kwa sababu wanajua timu zote zinahitaji kujiweka kwenye nafasi salama kwa kushinda michezo ya mzunguko wa kwanza.

Simba ilianza msimu huu kwa

INAENDELEA UK 23

# MAXI AFURAHIA REKODI YA MAYELE

●●● Afunguka bao lake laendelea kuwapaisha Wakongomani Yanga...



Maxi Nzengeli

Na Adam Fungamwango

KIUNGO mshambuliaji wa Yanga, Maxi Nzengeli, amesema amefurahia kufunga bao la kwanza la msimu kwa timu yake pamoja na kufikia rekodi iliyowahi kuwekwa na Wakongomani wenzake, Heritier Makambo na Fiston Mayele miaka ya nyuma, imefahamika.

Nzengeli anakuwa Mkongomani watatu kufunga mabao ya kwanza ya msimu kwa Yanga, baada ya kufunga bao la kwanza katika ushindi wa magoli 2-0 ambao waliupata ugenini dhidi ya Kagera Sugar, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba, mkoani Kagera Alhamisi iliyopita.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nzengeli alisema awali hakufahamu hilo kabla ya kuambiwa na watu wa kitengo cha habari na mawasiliano cha klabu hiyo.

"Nimefurahi sana kwa sababu nimekuwa mchezaji wa kwanza kufunga bao msimu huu katika kikosi chetu, lakini pia nimeambiwa nimefuata nyayo za Wakongomani wenzangu, kaka zangu, Makambo na Mayele ambao waliwahi kufanya kama mimi, kwa maana hiyo nimeendelea kupeperusha vyema bendera ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo hapa Tanzania," alisema mchezaji huyo.

Katika mchezo huo, Yanga ilishinda mabao 2-0, goli la pili likiwekwa wavuni na Mtanzania Clement Mzize, dakika mbili kabla ya mechi kumalizika.

Msimu wa Ligi Kuu 2018/2019, Makambo alikuwa mchezaji wa kwanza wa Yanga kufunga bao la msimu, akipachika bao katika mechi iliyofanyika Agosti 23, mwaka 2018, timu hiyo ikicheza dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Makambo alifunga bao dakika ya 30, mechi iliyoisha kwa Yanga kushinda mabao 2-1, goli la pili likifungwa na beki, Kelvin Yondani kwa mkwaju wa penalti wakati lile la kufutia machozi la Mtibwa Sugar likiwekwa wavuni na Haruna Chanongo.

Kwa upande wa Mayele, yeye alifunga bao la kufungulia msimu wa Ligi Kuu 2022/23 katika mechi ambayo Yanga ilicheza dhidi ya Polisi Tanzania, Agosti 16, mwaka

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >